

ULIMWENGU UNAPOROMOKA



Amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

² Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Baba yetu wa Mbinguni, sisi tena, usiku wa leo, tunakudhihirishia Wewe, Mwenyezi Mkuu, jinsi tulivyo na shukrani kukutanika hapa pamoja, tukiwa hai na tunaweza kukuabudu Wewe, usiku wa leo. Na sisi tumekuja pamoja kwa kusudi hilo, kuketi pamoja mahali pa Mbinguni, kama ndugu na dada, wenyeji wa Ufalme wa Mungu, tuingojea kuja kwa Roho Mtakatifu juu yetu, kwamba Yeye aweze kutufunulia kile tunachopaswa kufanya, mpango wa maisha yetu. Tunataka kutembea kulingana na mapenzi Yake.

³ Pia tunaomba, Bwana, kwamba Wewe utanzia kwenye msingi na kutusafisha tu, Bwana, na kutufanya viumbe vipya, kusudi tuweze kufaa kwa ajili ya huduma Yako. Tukijua kuwa hili haliwezekani kabisa kwetu, Baba; kwa kuwa hatuwezi kujitakasa wenyewe zaidi ya vile chui asivyoweza kuramba na kusafisha madoa yake, yeye huyafanya tu kuonekana zaidi kwa kujaribu kufanya juhudi zake mwenyewe. Lakini, “Kuna Chemichemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli.” Hiyo ndiyo husafisha madoa ya chui. Ninakuomba Wewe, Baba wa Mbinguni, kujalia, usiku wa leo, kwamba kila mmoja wetu anaweza kutumbukia chini Hapo, tukiacha mashaka yetu yote nyuma, mashaka yote ya upendo wa Mungu na ahadi kwa ajili yetu katika saa hizi. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

⁴ Hebu tuimbe huu tunapoketi chini. Badala ya kusema “amini tu,” hebu tuinue tu mikono yetu na kuimba “sasa naamini.” Naam, kila mtu sasa.

Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini;
Sasa naamini, sasa naamini,
Mambo yote yawezekana, sasa naamini.

⁵ Bwana awabariki, mnapoketi. Loo, linasikika la kufaa sana. Baada ya kumwomba Mungu, basi mwambie Yeye, “sasa naamini,” baada ya kumwomba Yeye.

⁶ Hii imekuwa ni siku ngumu kweli kwangu. Kuna mambo mengi sana ya kufanya, na labda mahojiano sabini na matano yanayongojea, na huwezi tu kuyafikia hayo yote, hivyo tu. Haiwezekani tu kabisa. Na nilikuwa na miito minne, leo, kuenda nje ya mji kwa ndege; mmoja kwenda Beaumont, Texas; na

mmoja kwenda Houston; na mmoja kwenda Campbellsville, Kentucky; na mmoja kwenda Little Rock, Arkansas, ugonjwa wa dharura. Na kabla tu ya kuondoka, kukaja mwito kwangu kusafiri kwa ndege kutoka hapa, Jumapili usiku, punde tu ibada ilipomalizika, kuwa mbali mahali fulani karibu na Pwani ya Magharibi, kuhubiri mazishi. Na huwezi kabisa kufikia yote. Na hilo ndilo tu lililoingia hapa, wale wanaojua kwamba tupo hapa; vipi kuhusu nyumbani, ofisini, mnaona? Na hao ni watu ambao ni watu wema. Na wao ni Wakristo, wengi wao. Na wao... Bali huwezi tu kuwa kila mahali kwa wakati mmoja, kwa hiyo unajaribu tu kufanya vizuri uwezavyo wakati ukiwa huko. Inakufanya kuwa na wasiwasi. Lakini unajua inahitaji watu wenye wasiwasi, wakati mwingine, kufikia mahali fulani, unajua, na wanapata kuchochewa kufikia mahali fulani.

⁷ Je! ulijua kwamba mara nyingi kwamba watu walio chini ya uvuvio huchukuliwa kuwa wendawazimu? Hiyo ni kweli. Wazia tu ni yupi kati ya manabii ambaye hakuchukuliwa kuwa mwendawazimu, unaona. Hata Yesu, walisema, “Wewe ni mwendawazimu,” maana yake *mwenye kichaa*, unaona. Na Paulo alisema, “Katika njia iitwayo ‘wazimu,’ hiyo ndiyo njia ninayomwabudu Mungu.” Unaona, *uzushi*, “wazimu.”

⁸ Na hebu wachukue washairi. Kwa ajili ya uvuvio, wanapanda kuingia mahali ambapo watu tu wa kawaida hawafiki huko. Ninawaza kuhusu—kuhusu Stephen Foster, ambaye aliipatia Marekani nyimbo zake maarufu za jadi. Sasa, nafikiri alikuwa nayo niani mwake, bali si moyoni mwake. Na mimi nilikuwa nikiishi ng’ambo tu ya mto kutoka makazi ya kale ya Kentucky. Unajua, baada ya kuandika wimbo ule maarufu wa jadi, angetoka na kuenda kulewa. Na asingeweza kabisa kustahimili. Na hatimaye huku akitoka chini ya uvuvio huo, siku moja, alimwita mtumishi na kuchukua wembe, na akajiua. Unaona, wewe—wewe ni. . .

⁹ Wakati ukiwa *huko* juu, kila kitu ni sawa, na wakati ukiwa *hapa* chini. Ni—ni katikati, wakati unaposhuka kutoka chini ya huo. Unapaswa kumwuliza meneja na baadhi yao ambao hujaribu kukutembeza usiku, baada ya mmoja wa mistari hiyo ya upambanuzi. Loo, jamani, hujui kama kila kitu ni ono, ama kinachofanyika. Hicho ni, unaona, kila kitu. Kila kitu unachotazama, hu—hujui kama kweli ni ono ama ni kitu gani. Unaninii tu. . . Na wewe ndiwe unafanya hilo. Unaona? Wewe ndiye—wewe ndiye yule hasa anayevuta hilo.

¹⁰ Nilikuwa nikieleza hilo kwa mchungaji, leo. Ni kama mvulana mdogo anayekaribu kuangalia kupitia shimo dogo ukutani, kuona sarakasi. Yeye huvuta kwa mikono yake, na kuangalia kupitia hapo, na anaweza labda kuona kama twiga au ngamia, na kuanguka chini tena. Na kusema, “Ni kitu gani kingine ulichoona?” Vema, karibu inamwua kuenda juu tena, kukiona. Lakini basi, baada ya kitambo, kama mtu mwingine

angeweza kuja karibu na kumchukua, amwinue juu, na kusema, “Hii hapa jinsi iendavyo. Sha—Shada la maua huanzia *hapa*, na la fahari ni upande *huu*, nalo hutokea *hapa*.” Humketisha chini. Mbona, halimsumbui.

¹¹ Hivyo ndivyo Mungu alivyokuwa ndani ya Kristo. Sasa yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, maskini mwanamke tu katika wakati wa kukoma hedhi, alikuwa anatokwa na damu. Na asingeweza... madaktari wasingeweza kukomesha hiyo. Na mwanamke huyo aligusa vazi Lake. Ndipo Yeye akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa Mimi? Nguvu zimenitoka Mimi.” Unaona, hiyo ilikuwa ni mwanamke huyo akitumia karama ya Mungu. Alimvuta Mungu kupitia Yeye. Hiyo ilikuwa ni huyo mwanamke akifanya hivyo. Alichukua fursa hiyo ya kutumia karama ya Mungu.

¹² Lakini, wakati Lazaro alipokufa, Yeye alisema Yeye hakufanya chochote mpaka Baba alipomwonyesha Yeye. Na baadaye, Yeye aliondoka kwa muda, ndipo—ndipo wao wakaagizia Yeye aitwe aje amwombee Lazaro. Yeye hakuenda; Yeye alienda mahali pengine. Ndipo basi wakatuma mtu tena. Na Yeye hakuenda; na kuikawilisha, akaenda mahali pengine. Na hatimaye akageuka, akawaambia wanafunzi Wake, “Lazaro analala.”

Vema, wakasema, “Anafanya vyema.”

¹³ Ndipo Yeye akaongea katika lugha yao, “Amekufa. Kwa ajili yenu, nina furaha sikuwa huko.” Unaona, Baba alikuwa amemwambia Yeye kwamba ingechukua muda gani, maana Yeye alisema kwamba hakufanya chochote mpaka Baba alipomwonyesha; na halafu ni muda gani ingechukua, na kile ambacho kingefanyika, na Kwake kurudi. Sikiliza tu. “Bali ninaenda kumwamsha.” Unaona?

¹⁴ Ndipo wakati Yeye alipofika chini kwenye kaburi la Lazaro, Yeye aliomba. Akasema, “Baba, ninakushukuru Wewe kwamba Wewe umesikia tayari; ila ninasema tu haya kwa ajili ya wale wanaosimama karibu.” Alijua kile alichokuwa anaenda kufanya, ndipo Yeye akamwita Lazaro kutoka kaburini. Hakukuwa na kitu kimoja kilichosemwa kuhusu nguvu kumtoka Yeye. Hiyo ilikuwa ni Mungu akitumia karama Yake, na ile nyingine ilikuwa ni mwanamke akitumia karama ya Mungu.

¹⁵ Sasa, huwezi kutengeneza ono. Inabidi litoke kwa Mungu.

¹⁶ Kwa hiyo imani yako ndiyo inayofanya hiyo. Imani ndiyo kitu pekee ambacho Mungu atatambua, katika kiumbe, ni imani katika Neno Lake lililoahidiwa, na unafanya hilo mwenyewe. Ni imani yako ndiyo inayofanya hilo. Lakini basi wakati ono likija, wakati mwingine, ono ambalo Mungu angetoa kuhusu kuenda mahali fulani, mbona, wakati mwingine linachukua saa nyingi, kamwe halinisumbui. Bali ni aina hizi ndizo huumiza, halafu unarudi na unashangaa mahali ulipo.

17 Nafikiri William Cowper, ninaamini, lilikuwa ndilo jina lake, aliandika *Kuna Chemichemi Iliyojaa Damu*. Nilisimama kando ya kaburi lake, si muda mrefu uliopita, huko London. Inilazimu tu kulia kidogo, kwa sababu nilimhurumia mtu huyo. Alikuwa ni mshairi. Na yeye, wakati alipopanda juu katika uvuvio na kuziandika nyimbo hizo. . . Vema, alipoondoka kwenye huo, a—alijaribu ku. . . alikuwa na de—dereva na akajaribu kutafuta mto, kujiua, na kulikuwa na ukungu sana wasingaliweza hata kuupata. Unaona, ali—alipotea, alikuwa amekuja kutoka kwa uvuvio, kurudi chini duniani tena.

18 Hayo yote yanamaanisha nini, rafiki? Kwamba kweli kuna Nchi ng'ambo ya mto, inakubidi tu kupanda juu kuiona Hiyo. Kwa hiyo tunajua inaenda kuwa siku moja ambapo sisi tutaenda kwenye Nchi hiyo. Hilo ndilo Tumaini letu kubwa.

19 Sasa, usiku wa leo, kamwe sikumwambia mwanangu kutoa kadi za maombi. Lakini kila usiku Bwana amekuwa akiwaponya wagonjwa kutoka kwenye kusanyiko, na kuwaita tu, wale walio na imani. Sikiliza kwa makini kile Yeye asemacho sasa, unaona, na wakati Yeye—wakati Yeye anapozungumza.

20 Bali nafikiri, kesho usiku, sasa, kwamba tutabadilisha u—utaratibu wa mkutano. Na ni wangapi wangetaka kuombewa tu, ku—kuombewa tu, wagonjwa? Vema, sawa. Nitamtuma Billy, mapema tu kidogo, kama ni sawa na mchungaji wetu mpendwa, na tutawapeni, nyinyi nyote, kadi ya maombi, anayeitaka, na ndipo tutaita tu watu wote, na kuja karibu na kuwaombea.

21 Nisingeweza kuchukua kila mmoja katika moja ya mistari hiyo ya upambanuzi. Ninge. . . wangukuwa wananitoa nje, na nyinyi mangukuwa mnaniombea. Na—na hebu wazia tu, kama mwanamke mmoja aligusa vazi Lake. . .

22 Na Yeye alikuwa ni Mwana wa Kiungu wa Mungu. Kama mwanamke mmoja aligusa vazi Lake na ilimfanya Yeye kujihisi mnyonge, ingenifanya nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Usingeweza kumaliza mmoja, ama labda hiyo, kama Yeye hakuwa amesema, “Mambo haya niyafanyayo, nyinyi nanyi mtayafanya; mengi kuliko haya mtafanya.” Kwa kuwa, unaona, Yeye alisema, King James ina “kubwa zaidi,” bali neno sahihi ni “mengi zaidi,” ukilichunguza, “mengi zaidi.” Maana, hakuna mtu angaliweza kufanya kubwa kuliko hayo; Yeye alifufua wafu, na kusimamisha maumbile. Alifanya kila kitu. Kwa hiyo kitu pekee, Kanisa. . . Mungu wote alikuwa ndani ya Mtu mmoja hapo, lakini ile Nguzo kubwa ya Moto iliyowaongoza Israeli ilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu.

23 Lakini wakati Yeye aliposulubiwa, akafufuka tena na kupaa juu kwa Mungu; kwenye Siku ya Pentekoste, Yeye alirudi katika umbo la Nguzo hii ya Moto, na kujigawa Mwenyewe, ndimi za Moto zilikalia juu ya kila mmoja wao. Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwa Kanisa Lake, maana huyo alikuwa ni

Mke Wake. Na mume na mke ni kitu kimoja, kwa pamoja. Naye Mungu na Kanisa ni kitu kimoja, kwa pamoja. Mungu ndani yako! Huyu alikuwa ni Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, Mungu ndani yetu, Mungu yeye yule wakati wote; madhihirisho matatu tu, sifa, au ofisi, ama chochote utakacho kukiita hicho. Kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Huyu ni Mungu yule yule wakati wote. Unaona?

²⁴ Na sasa huyo alikuwa ni Mungu juu yetu, asingeweza kuguswa. Hata mlima ambao ungeguswa, mahali Yeye alipokuwa, hawana budi kuchomwa kwa mkuki, maana dhambi haikuwa imekuwa na sadaka bado.

²⁵ Lakini basi Mungu akaja na alidhihirishwa miongoni mwetu, “Sisi tulimghusa Yeye kwa mikono yetu,” alisema, “Mungu!” Timotheo wa Kwanza 3:16, “Bila pingamizi siri ya utauwa ni kuu; kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na Malaika, na kuaminiwa ulimwenguni, akapokelewa juu Utukufuni.” Unaona? Unaona, sasa, huyo alikuwa ni Mungu pamoja nasi.

²⁶ Mungu juu yetu, Mungu pamoja nasi, sasa Mungu ndani yetu. Yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamimina ndani ya Kristo; yote aliyokuwa Kristo, Yeye aliyamimina ndani ya Kanisa. “Katika siku hiyo, mtajua ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, na nyinyi ndani Yangu.” Kwa hiyo imekuwa ni Mungu kila wakati, unaona, kazi Zake zile zile. Kanisa limekusudiwa kuendeleza kazi Yake, pamoja na Roho yule yule. Usingeweza kuendeleza kazi ile ile bila ya Roho yule yule. Hiyo ni kweli. Roho yule yule huendeleza kazi.

²⁷ Kwa hiyo sasa nyinyi ni wazuri sana kuzungumzia, ni—ninapitiliza wakati, kila usiku. Na mimi—mimi sipendi kufanya hivyo.

²⁸ Bali nafikiri, kwa moyo wangu wote, kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Si—sininii—sisemi hilo kwa sababu tu ni msemu wa kawaida miongoni mwa watu. Ninaliamini. Ninaliamini kwa moyo wangu wote, na kwa uaminifu ndani ya moyo wangu. Hiyo ndiyo sababu sijaribu kujenga vitu vikubwa, kufanya mambo makubwa mashuhuri, na kujenga minara mikubwa iliyochongoka na kadhalika. Na ni—ninaamini Kristo anakuja. Mimi—mimi. . . Kila kitu, hebu—hebu tukifanye sasa hivi, kwa sababu huenda kusiwe na kesho, unaona. Hebu tukifanye leo, kama tunaweza, kila kitu tuwezacho kufanya.

²⁹ Hivyo basi sikuruhusu kamwe, ama sidhani Roho Mtakatifu angenitaka niwe na vitu vikubwa mashuhuri, ambapo ingekuwa na ninii kubwa mashuhuri. . . Sasa, hilo ni sawa kwa wale ambao wanataka kufanya hivyo. Siwahukumu. Hilo ni sawa. Bali kuwa na kama matangazo ya televisheni ambayo hujumuisha taifa lote, inibidi kuwaomba watu fedha; na kufanya hivyo, inawabidi kufanya hivyo, maana inawabidi kulipia hayo.

Matangazo ya redio, hayo ni—hayo ni sawa, hilo ni jema, lakini hilo halikuwa kwa ajili yangu mimi. Ninapenda tu... Mbona, ningehangaika hata kufa, juu ya hayo. Na nisingeweza kufanya hilo. Nisingeweza.

³⁰ Nilianza kuchukua sadaka, wakati mmoja maishani mwangu. Nadhani mlisikia kuhusu hilo. Ni—nilianza kuchukua sadaka. Tuliingia tu katika hali ngumu, mpaka karibu ilinibidi kuchukua. Ni—nilikuwa na madeni fulani, na nilikuwa ninafanya kazi. Nilichukua kofia yangu na kumwaga mshahara wangu, na hatungeweza kabisa kumudu. Na kamwe sikuchukua toleo kwenye Maskani. Nilikuwa mchungaji miaka kumi na saba, bila senti. Ndipo nikamwambia mke wangu, nikasema, “Sisi, inatubidi tu kufanya hivyo. Ninaenda na kuchukua sadaka.”

³¹ Akasema, “Ninaenda kukuangalia, unaona.” Unaona? Anaenda na kuketi chini.

³² Basi usiku huo, baada... Wao ni watu wenye upendo. Bariki mioyo yao. Nikasema, “Kwa—kwa namna fulani ninachukua kusema hili.” Nikasema, “Nimekuwa pamoja nanyi kwa muda mrefu. Kamwe sikuwaomba chochote,” nikasema, “lakini ni—niko na gharama fulani inanibidi kulipa. Ninahitaji kama dola sita.” Ndipo nikasema, “Si—sijaipata tu. Sijapata, na inafaa kulipwa,” ndipo nikasema, “Jumamosi. Na si—sina hiyo kulipa.” Na nikasema, “Kama nyinyi nyote, yeyote wenu aliye na yapata peni moja,” nikasema, “kama ungesaidia kidogo kwa hiyo, nitathamini hilo.” Na—na kila mtu akaanza kulia. Kulikuwa na mwanamke mkongwe aliyeketi chini hapo... Ndipo shemasi akasimama, na hata hatukuwa na sahani ya kukusanya, ndipo ni—nikasema, “Unaweza kuchukua kofia yangu.” Na akaenda akaichukua kofia yangu.

³³ Na nikaangalia pale chini. Na maskini dada mkongwe daima ananiombea, alikuwa na... Mmoja wa hawa mama wa kusini wa mtindo wa kale waliokuwa na mmoja wa maskini hivi... vijitabu vidogo vya mfukoni ambavyo hufungwa sehemu ya juu. Alifikungua hicho, na, loo, jamani! Nilitazama hicho. Nisingeweza kutumia hiyo bure. Nikasema, “Ni—nilikuwa tu nikitania. Nilitaka kuona kile mlikuwa mnaenda kusema. Sikumaanisha hilo hasa.” Nisingeweza kufanya hilo. Hapo ndipo nilipoweza kufikia karibu sana na kuchukua sadaka. Unaona?

³⁴ Kulikuwa na mzee aliyezoea kuja huko chini nyumbani kwangu. Yeye—yeye, nafikiri alikuwa ni wa Nyumba ya Daudi, ama kitu fulani. Alikuwa na ndevu kubwa na nywele. Alinipatia baiskeli kuukuu, kwamba iliharibika; lakini si kuharibika, ilichakaa tu. I—ilikuwa labda imetumikia wajibu wake vizuri, lakini ilikuwa... Kwa hiyo ni—nilienda chini kwenye duka la bei rahisi na kujinunulia mikebe miwili ya rangi, kwa senti ishirini, na nikaipaka rangi na kuiuza dola sita. Kwa hiyo haikunibidi

kuchukua sadaka, unaona. Kwa hiyo hapo ndipo nilipokuja karibu sana. Mimi—mimi . . . Unaona?

³⁵ Vipi kama ningalikuwa hapa na jukumu hilo kubwa lote, na Roho Mtakatifu aliniita kutoka mahali fulani kwenda kwenye kanisa dogo, ambapo labda ingenibidi kuwa na mamia ya dola kwa siku moja, kulihudumia hilo? Wasingeweza kufanya hilo. Lakini, unaona, sihitaji chochote ila tu Mungu zaidi. Unaona? Si—sihitaji. Kwa hiyo kama Yeye akiniita mahali popote, haijalishi ni wapi, kama kuna watu kumi ama . . . Na mimi nimewahubiria laki tano, kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, vema, wakati wowote ikifikia hapo, mtu fulani anaweka tu . . . Mungu huliweka moyoni mwao, na wanakuja karibu na kusema, “Unajua, Bwana alisema ulikuwa unaenda mahali fulani, na hii hapa hundi kwa ajili yake.” Hiyo ndiyo, kwa imani, unaona, kwa kuwa Yeye anajua kile tunachohitaji. Unaona? Na kwa hiyo ninapenda tu kuishi namna hiyo.

³⁶ Na halafu kitu kingine, unajua, ninafikiri tunaenda chini mahali mbalimbali. Watu wengi ambao huja katika mikutano yangu ni watu maskini kama tu mimi, na ninataka kubakia tu kama walivyo. Hivi ingeonekana sawa sasa kwa mhudumu kuzunguka, kitu fulani kikubwa sana, mwajua, namna hiyo, na makumi elfu ya dola, na kuitupa upande *huu* na upande *ule*; na—na mwanamke fulani maskini akikokota gunia la pamba mgongoni mwake, akichuma pamba kwa yapata dola tatu kwa siku, akila mafuta ya nguruwe na ugali wa mahindi? Ha-ha. Siwezi, siwezi kuona hilo, unaona. Kristo alimiliki dunia, na hakuwa na mahali pa kuweka kichwa Chake; “mbweha wana mapango.” Na Yeye alikuwa Mfano wetu. Yeye alikuwa kile Yeye alichopaswa kuwa.

³⁷ Sasa, si kama ninajaribu bado kukosoa hilo. Ninajaribu tu kuwaambia kunihusu mwenyewe. Hivyo basi, bila ya fedha, basi sijawahi kujaribu kuanzisha kitu chochote kikubwa, mwajua. Na—na huwezi kuanzisha chochote kikubwa, hata hivyo. Kitu kikubwa kuliko vyote kilichoko, tunakiendea Hicho, unaona; kwa hiyo, na hicho ni Mungu. Na mimi ninafikiri sote tu wa saizi moja, na hebu tukae tu namna—namna hiyo. Sisi ni watoto wa Mungu.

³⁸ Sasa, ni—ninapenda tu kusoma Biblia hii. Na siwezi kuisoma vizuri sana na wakati mwingine mimi hutamka maneno yangu vibaya, bali mtavumiliana nami kwa hilo. Mimi—mimi—mimi . . .

³⁹ Wakati mmoja ninakumbuka ilikuwa huko Fort Wayne, nilikuwa nikihubiri. Na kulikuwa kumekuwa na Assemblies of God walibeba makala haya, na ndipo *Watu Mashuhuri* wakayapata; msichana mdogo. Huenda mliisoma yapata miaka kumi iliyopita. Walikuwa, alikuwa ame . . . macho yake yalifanyiwa upasuaji na uwezo wake wa kuona ukatoweka.

Na—na yeye akaletwa ndani kwangu, ndipo Roho Mtakatifu akamwambia yote kuhusu hilo na kumponya papo hapo; angeweza kusoma Biblia au chochote. Ndipo *Watu Mashuhuri* wakaichukua. Hicho kitabu, unajua, wale *Watu Mashuhuri*, katika sayansi ya tiba na chochote zaidi, ambacho aliweza.

⁴⁰ Na ninakumbuka, siku kadhaa usiku baada ya hapo, nilirudi huko nyuma ambapo Paul Rader aliandika ule wimbo, *Amini Tu*. Na nilikuwa nimeketi hapo na kusikia huo ukiingia. Kulikuwa na m—mtu ambaye alikuwa na elimu kwelikweli, lazima alikuwa nayo, na kwa hiyo akarudi nyuma, akasema, “Bw. Branham, je! ninaweza kuongea na wewe?”

Nikasema, “Naam, bwana.”

⁴¹ Ndipo akajitambulisha mwenyewe, na—na yeye akasema, “Ninataka tu kukusahihisha juu ya mambo fulani.”

Nikasema, “Vema, bwana.”

Ndipo akasema, “Sarufi yako.” Unaona?

⁴² Nikasema, “Naam, bwana, ninajua hiyo.” Nikasema, “Mimi ninayo tu elimu ya daraja la saba.” Nikasema, “Tulikuwa na watoto kumi. Baba yangu alikuwa mgonjwa mgonjwa na ilinibidi kuenda kufanya kazi. Ilinibidi kuacha shule, mvulana mdogo tu.”

Alisema, “Hiyo si kisingizio sasa.”

⁴³ Na mimi nikasema, “Hiyo, hiyo ni kweli.” Nikasema, “Nadhani siyo. Lakini sasa kwa kuwa nimeingia kumtumikia Bwana, sina wakati kufanya hivyo, kwa lolote la hilo.”

⁴⁴ Akasema, “Vema, ninii yako...” Kasema, “Watu kule nje!” Kasema, “Nilikuona jana usiku, ulisema, ‘Nyinyi watu wote mnaokuja hapa karibu na mimbara hii,’ kasema, ‘nenda chini...’”

⁴⁵ Ndipo nikasema, “Vema, kitu gani? Sikujua tofauti yoyote.” Na yeye akasema... nikasema, “Kuna shida gani na hiyo?”

⁴⁶ Kasema, “Si mimbara,” kasema, “ni *mimbara*.” Akasema, “Kusanyiko lako lingekuthamini zaidi kama ungesema *mimbara*.”

⁴⁷ Vema, nafikiri kwa namna fulani alizichana nywele hizo chache vibaya. Nikasema, “Ndugu,” nikasema, “Sitaki kutofautiana na wewe. Bali siamini watu hao hujali kama nikisema mimbara au *mimbara*, ili tu kwamba nihubiri Neno la Mungu, na kuishi maisha yaliyo ndani ya Hili.” Hilo ndilo jambo kuu. Amina.

Maskini jamaa huyo akasema, “Lakini huijui Biblia yako.”

⁴⁸ Nikasema, “Bali ninamjua Mwandishi vizuri sana, na Yeye—Yeye hunibariki.” Afadhali nijue, “kumjua Yeye ni Uzima.” Unaona?

⁴⁹ Sasa, kesho usiku, uje mapema kidogo. Kwa sababu, nikija, dakika chache tu zilizopita, ndani ya teksi huko nje, kulikuwa tu na milolongo ya watu, wameudhika, wengine wakilia, wakiondoka mahali hapo, na walikatazwa kuingia. Kwa hiyo njoo mapema uwezavyo, kupata kadi yako ya maombi.

⁵⁰ Sasa kabla tu hatujaangalia kwenye Neno, hebu tuzungumze na Mwandishi kwa dakika moja.

⁵¹ Baba wa Mbinguni, hili ni Neno Lako. Na tunasoma katika Biblia, kwamba, "Tunaoshwa kwa maji ya Neno." Na sisi tunajua, katika Agano la Kale, jinsi walivyomchukua ndama, ndama mwekundu, na kumwua, kusanyiko lote, na aliteketezwa. Na ndipo majivu yakawekwa nje ya mabaraza, kwa ajili ya maji ya farakano, kwamba—kwamba mikono iliyogusa hili lazima iwe mikono safi. Na ni—ninakuomba Wewe, Mungu, kama vile maji haya ya farakano, Neno ambalo hututenga kutoka kwa mauti, kuingia Uzimani; takasa mawazo yetu, mioyo yetu, Bwana. Na ikiwa kuna chochote ambacho Wewe unaona ndani yetu, ambacho si sahihi, kisafishe, Bwana, kwa maji haya ya farakano, usiku wa leo. Ondolea mbali dhambi zetu, Baba. Sisi—sisi tunataka kusimama kila siku mbele Zako, tukifa kwa nafsi zetu, kusudi tuweze kuishi ndani ya Kristo. Bariki Neno tunapolisoma Hilo. Pia Wewe uliahidi kwamba Hilo lisinge—lisingerudi bure, bali Hilo—Hilo lingetimiza kile ambacho lilipaswa kufanya. Na sisi tunaomba kwamba Wewe utajalia hili kupitia Jina la Yesu. Amina.

⁵² Katika Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo, tunakuta ninaenda kusoma kidogo tu kutoka Muhuri wa Sita. Kutoka kwenye Kitabu cha Ufunuo, unaopatikana katika mlango wa sita wa Ufunuo, na halafu tutaanza na kifungu cha 12. Na halafu pia ninataka kusoma kutoka Waebrania 12:25, pia, kwa ajili ya nukuu nyingine ndogo, kwa ajili ya Maandiko fulani niliyoandika hapa chini. Na ma—mambo machache ningependa kuzungumzia, Bwana akipenda. Na sasa juu ya Ufunuo 6:12.

Nami nikaona, alipofungua muhuri ya sita, na, tazama, palikuwa na tetemeko kuu la nchi; jua likawa jeusi kama gunia la singa, mwezi wote ukawa kama damu,

Na nyota za mbingu zikaanguka juu ya nchi kama vile mtini upukutishavyo mapooza yake, utikiswapo na upepo mwingi.

... mbingu zikaondolewa kama ukurasa ulivyokunjwa; na kila mlima na kila kisiwa kikahamishwa kutoka mahali pake.

Na wafalme wa dunia, na wakuu, na matajiri, ... majemadari, na wenye nguvu, ... kila mtumwa, na kila mwungwana, wakajificha katika ... mapango na katika ... miamba ya milima.

Wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo.

Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yake imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?

⁵³ Sasa katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 12, na kuanzia kifungu cha 25.

Angalieni nyinyi msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyenena juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka, sisi tukijiepusha na hilo, na yeye anenaye kutoka mbinguni;

Ambaye sauti yake iliitetemesha nchi wakati ule; lakini sasa ameahidi, akisema, Naam, mara moja tena nitatetemesha si nchi tu, bali na mbingu pia.

Lakini neno hili, Mara moja tena, ladhihirisha... kuhamishwa vile viwezavyo kutetemesha vikae, kama vitu vilivyowmbwa, vitu visivyoweza kutetemesha vikae.

Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemesha, na tuwe na neema, ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho;

Maana Mungu wetu ni moto ulao.

⁵⁴ Sasa hili ni fu—fungu dogo ambalo ningependa kutoa kutoka hapo, kufanya fungu kutoka kwalo, kama ninaweza kuliita. Na ninatumaini siwaweki muda mrefu kupita kiasi. Na kwa hiyo msisahau kesho usiku, sasa, kuja mapema kupokea kadi za maombi, na tutakuwa na mstari wa maombi ambapo tunaombea watu wote walio na kadi za maombi. Sasa, na somo langu usiku wa leo ni *Ulimwengu Unaporomoka*. Ni somo la kipekee sana.

⁵⁵ Bali nilikuwa nikiwazia leo, vile nilikuwa na fursa kuu na majaliwa makuu kutembea na Ndugu Vick, mtumishi huyu wa Kristo, mwenye heshima na mwadilifu; pamoja na Ndugu Joseph, rafiki yangu wa thamani, pia. Tulikuwa na, vema, ilikuwa ni chakula cha jioni, kwangu mimi. Nafikiri ni chakula cha mchana, kwenu nyote hapa. Lakini kama hicho ni chakula cha jioni, basi hiki ni chakula cha jioni usiku wa leo, na hicho ni chakula cha mchana na kiamshakinywa, chakula changu cha jioni kinaingilia wapi? Unaona, ninajisikia kwamba nimeacha kitu. Na halafu tulipoenda kwenye—kwenye chakula cha jioni na kurudi kuteremka mtaani, tulikuwa tunatambua walikuwa wanaandaa, wanaanza kuandaa vitu kwa ajili ya Krismasi. Tunakaribia majira ya Krismasi, na moja kwa moja ni mwezi mmoja unaokuja, lakini maduka yote yanamaliza mauzo yao ya Krismasi.

⁵⁶ Jinsi wanavyokosa kwa mbali maana ya Krismasi! Limekuwa tu ni tukio la biashara. Sikukuu zote zimekuwa hivyo; Siku ya Mama, Siku ya Baba. Na kila siku inapaswa kuwa ni siku ya mama na baba. Na wao wana, loo, Pasaka. Baba Krismasi alichukua—alichukua mahali pa kuzaliwa. Sungura na kuku, maskini bata, alichukua wakati wa ufufuo. Ni kuku wote na mabata na mayai, na hayo yana uhusiano gani na ufufuo? Unaona? Na ni vibaya sana sisi. . . hiyo inaiweka mbele za watoto wetu.

⁵⁷ Wavulana wengi wadogo hapa nje, usiku wa leo, wanaweza kukuambia mengi kuhusu Davy Crockett kuliko anayoweza kukuambia kuhusu Yesu Kristo, hakika, hakika, kwa sababu ni jambo kuu la kibiashara. Wanachukua nguo kama kaoboi fulani au shujaa fulani, na, ama kitu fulani au haramia fulani au kitu fulani, na—na wanauza nguo ambazo zinaonekana kama yeye, na—na halafu watoto wadogo wote wanajua kuhusu hilo na kusoma historia yake. Laiti tungeweza tu kuwapatia watu mpango wa Kristo, namna hiyo. Kwa kawaida unajaribu kuiga kile unachosoma; nyinyi, wasomaji.

⁵⁸ Ninakumbuka, imekuwa daima imekuwa hivyo kwangu. Ninakumbuka wakati mmoja, kama mvulana mdogo, yapata miaka kumi na miwili, chini katika maktaba ya umma, nilichukua moja ya vitabu vya Zane Grey kiitwacho *The Lone Ranger*. Ni—niliendesha farasi mpya wa mama kwelikweli, kama farasi wa kuchezea kwenye bembea, kuzunguka na kuzunguka nyumba, mpaka nikamvunja. Baadaye, nilisoma hadithi ya Edgar Rice Burroughs ya *Tarzan Na Manyani*, na nikalala kwenye mti, kwa sababu ni—ni—nilikuwa ninasoma hiyo. Hiyo ilikuwa niani mwangu.

⁵⁹ Na, loo, siku moja nilipata kitu kilichokuwa halisi, Kweli, si hadithi ya kubuni. Na tangu wakati huo, ninataka maisha yangu yawe kama Yake. Nilipata kitu fulani ambacho kilikuwa halisi wakati niliposoma Biblia na maisha ya Yesu Kristo.

⁶⁰ Sasa tunapokaribia majira haya, inajulikana sana. Ulimwengu karibu uko tu katika hali ile ile uliokuwa miaka elfu mbili iliyopita, wakati Yeye alipokuja duniani katika kuja Kwake kwa kwanza. Wakati Yeye alipokuja duniani, dunia ilikuwa imetimiza wakati wake. . .

⁶¹ Kila mara kwa mara ulimwengu huingia katika hali ya mchafuko mpaka hakuna kitu kiwezacho kuusaidia. Tumekuwa na hii mara kadha, tangulizi hizi. Na sisi—sisi tunaona kwamba kila wakati ukiingia katika hali hii, na, hufanya watu ku—kuanza kuomba. Na wao wanahisi kwamba kila kitu kimejidhihirisha, kama vile mifumo yetu yote na kila kitu tulicho nacho, hujidhihirisha chenyewe hadi mwisho. Ilifanya hivyo katika ulimwengu uliotangulia gharika, na kadhalika. Siasa na—na vitu vingine hufikia tu mwisho wake,

hakuna chochote kwake tena. Na mimi—mimi nafikiri yote yanayofanywa na Mungu, kwa kusudi, ili kwa namna fulani kurudisha nguvu za ujana, ili kwa namna fulani kurudisha. Daima ina njia ya kujifanya upya. Na mimi ninafikiri ni ka—kanuni tu ya Mungu, kwamba mambo haya hufikia mahali hapo.

⁶² Wakati wa kuja kwa kwanza kwa Kristo, ni—ninaamini tunaweza kusema ulimwengu ulikuwa unaporomoka. Ulikuwa ni wakati mwovu katika siasa, wakati mwovu katika—katika dini. Mifumo yote ilikuwa imechafuka. Walikuwa wamechanganya ndani, wakiingiza mambo mengine na mawazo ya kubuni ya wanadamu, katika dini, na kadhalika, mpaka kitu chote kikachafuka. Na ulimwengu ulikuwa unaporomoka.

⁶³ Nao ulimwengu, kwenye wakati huo, ulikuwa ukiomba kwa ajili ya masihi. Sasa, Warumi walikuwa wakiomba kwa ajili ya masihi, Wayunani walitaka masihi, Wayahudi walitaka masihi. Na Mungu akawapa Masihi, bali hawakuitaka katika njia ambayo Yeye alituma.

⁶⁴ Nami nashangaa leo hii, katika wakati wetu wenye mchafuko, kwamba ikiwa sisi sote tunafikia mahali hapa tena, tunapokaribia Krismasi, tunakuta ulimwengu karibu katika hali iyo hiyo; umeoza kimaadili, na siasa imeoza, maisha ya kidini ya—yameoza, umadhehebu umeoza, na kila kitu kimeoza kabisa. Na sisi sote tunatazamia kitu fulani kutusaidia kutoka kwake. Sisi sote tunatarajia masihi.

⁶⁵ Sijui, kama Mungu alitutumia Masihi, kama tusingalifanya tu jambo lile lile walilofanya wakati uliopita. Tusingalimjua Yeye, tusingalijua kuwa Yeye alikuwa ni Nani. Sidhani kama ulimwengu ungemtambua Yeye, hata kidogo.

⁶⁶ Basi tazama ni kwa nini. Hili hapa wazo langu, sababu yake. Warumi, walikuwa na wazo lao la kile masihi anapaswa kuwa. Kila mmoja wetu analo wazo letu wenyewe; kila dhehebu lina mawazo yake. Tumefunzwa, tukachora kwenye chati na kila kitu, kile Masihi anachopaswa kuwa, jinsi inavyoenda kuwa, “Kanisa letu ndilo linaloenda kupokea Hilo.” Vema, Wayahudi, Mafarisayo walifikiria hilo, na vivyo hivyo na Masadukayo walifikiria upande wao. Jambo lile lile, unaona. Roho hazi; mtu tu aliyekaliwa. Unaona? Kwamba, ibilisi hachukui roho yake, humchukua tu mtu huyo. Na jambo jema kuhusu hilo, Mungu hachukui Roho Wake, pia, unaona, Huyu hubaki; mtu tu. Roho yeye yule aliyekuwa juu ya Kristo yuko juu ya mwaminio leo hii, mwaminio wa kweli.

⁶⁷ Sasa tazama, Warumi katika siku hiyo walikuwa wakitazamia ma—masihi, mwa—mwanasiasa. Walitaka mtu ashuke kutoka Jupiter, ama mtu fulani kushuka akiwa na gari la moto la kukokotwa na farasi, na—na jua nyuma ya kichwa chake, na angeyavuta magari ya kukokotwa na farasi kupitia angani. Na walitaka Jupiter kushuka na kuwafanyia vitimbi,

siri ya kijeshi jinsi wangeweza kukanyaga na kuondolea mbali ulimwengu wote. Hilo ndilo walilotaka kufanya. Walitaka kuwapiga Wayunani, na—na kutawala ulimwengu mzima. Huyo ndiye aina ya masihi waliyemtaka.

⁶⁸ Vema, Wayunani walitaka masihi wa aina hiyo aje na kuwaambia hasa aina ya mbinu ambayo wangeweza kutumia kuwapiga Warumi. Unaona, hiyo ndiyo aina.

⁶⁹ Nao Wayahudi, walikuwa wakimtazamia Jemadari, mtu fulani ambaye alikuwa anakuja na fimbo ya chuma mkononi mwake, na Simba wa Kabila la Yuda, na alikuwa anaenda kutawala mataifa yote; na kufukuza Rumi huko nje kuingia mtoni na kuwazamisha, na—na—na Israeli ilikuwa inaenda kuchukua mamlaka. Hiyo ndiyo sababu. Wakati alipokuja hasa jinsi Maandiko yalivyosema Yeye angekuja, bali walikuwa wanamtazamia Yeye kwa njia tofauti.

⁷⁰ Nashangaa kama isingekuwa ni jambo lile lile leo hii, kama Yeye akija, kama tusingeweza kuwazia hilo. Tunayo mawazo yetu wenyewe kuhusu kile Yeye anachopaswa kuwa, na jinsi Yeye anavyopaswa kuonekana, na jinsi Yeye anapaswa kuvaa nguo Zake, na kugawa nywele Zake, na kila kitu. Kama si tu ladha yetu, mbona, tusingeipokea, unaona; ninamaanisha, sisi, ulimwengu leo hii, unaona. Vema.

⁷¹ Wao—wao, Wayahudi, walimkataa Masihi, kwa sababu kwamba Yeye hakutoshea ladha yao. Hakutoshea.

⁷² Siku chache zilizopita, mshona nguo mzuri huko Tucson alikuwa ananikatia suruali fulani. Na yeye alikuwa ni Myahudi. Na nikasikia Kiingereza chake kibovu, ndipo—ndipo nikasema, “Wewe ni nini, Myahudi?”

⁷³ Akasema, “Naam, bwana.” Naye akasema, “Nadhani wewe ni Mkristo?”

⁷⁴ Nikasema, “Naam, bwana.” Kwa hiyo akaendelea kutengeneza suruali yangu. Na mimi nikawazia, “Nitamwacha aongoze wakati unaofuata.”

⁷⁵ Ndipo yeye akasema, “Vema,” akasema, “Sina chochote dhidi yenu Wakristo.”

⁷⁶ Nikasema, “Asante, bwana. Sina chochote dhidi yako.” Ndipo yeye akasema, akasema ninii . . . nikasema, “Ni nini maoni yako kumhusu Kristo?”

⁷⁷ Akasema, “Alikuwa mapema sana, na wao walisema Yeye alikuwa kijana sana kwa kazi hiyo.”

Na mimi nikasema, “Naam, bwana.”

⁷⁸ Akasema, “Yeye alikuwa tu kidogo ni kijana kupita kiasi kwa ajili ya kazi Yake.” Kasema sasa, Kristo, “Kama Yeye, Yesu, angalikuja leo hii . . .” Si Kristo; hawaamini hilo. Kasema, “Kama Yesu angalikuja leo hii, mpango Wake ungalikuwa sawa.”

Kasema, “Ni jambo fulani, lingine, kama vile Rockefeller na Goldwater,” kasema, “wanapigana mmoja na mwenzake, na ndani ya chama kimoja.” Na yeye akasema, “Unaona, wao—wao hawapaswi kuwa wakifanya hivyo.”

Nikasema, “Hilo ni sahihi.”

⁷⁹ Kasema, “Wakati Yesu alipokuja,” kasema, “Alikuwa akipiga vita chama Chake Mwenyewe, watu Wake.”

⁸⁰ Nikasema, “Loo, la. Alikuwa kwa walio Wake Mwenyewe, na walio Wake Mwaneyewe hawakumpokea Yeye.” Nikasema, “Hilo, hilo lilikuwa ndilo, unaona.”

⁸¹ Kwa hiyo nitamwacha apumzike mpaka nitakaporudi, unaona, kwa namna fulani kidogo kidogo kila wakati. Kwa sababu, ninakumbuka Mungu alipofusha macho yake kusudi mimi niweze kuona, unaona, kwa hiyo ni—nina shukrani sana kwa jamii hiyo. Hakika nina shukrani. Usiwe na wasiwasi, Israeli, kama umeketi hapa, wakati wenu utawadia hivi karibuni. Unaona? Hakika.

⁸² Sasa mara nyingi tunasema kwamba, “Yesu alikuwa Myahudi.” La. Hakuwa. La, Yeye hakuwa Myahudi. Hakuwa Myahudi wala Mtaifa. Yeye alikuwa ni Mungu. Unaona, himoglobini ndipo seli ya uhai ilipo, na seli ya uhai ilikuwa ni seli umbivu kupitia Mungu. Hakukuwa na—na maisha ya kijamii kati ya Mungu na Mariamu. Hakuna hata msisimko. Aliumba seli zote mbili, hiyo ni kweli, yai na seli. Na Yeye alikuwa si Myahudi wala Mtaifa. Yeye alikuwa ndiye lile pengo, katikati. Yeye alikuwa ni Mungu. Na kama Yeye alikuwa ni damu ya Myahudi, tumepotea; kama Yeye alikuwa damu ya Mtaifa, tumepotea. Yeye alikuwa ni Damu ya Mungu, aliyeumbwa bila tamaa ya kujua kimwili. Hiyo ni, hiyo ndiyo sababu imani yetu inaweza kutazamia Kule na kusimama kwa hakikisho hilo Ndilo. Kwa hiyo Yeye alifia wote wawili.

⁸³ Sasa tunaona kwamba wakati Yeye alipokuja, hata hivyo, Yeye hakuja katika ladha ya Myahudi, kwa hiyo wao walimhukumu Yeye. Na sasa sisi—sisi hatuwezi kusema chochote juu yake, kwa sababu tunafanya jambo lile lile.

⁸⁴ Ni kitu gani kilichosababisha hili? Ninaamini kulikuwa na kisababishi cha hilo. Na mimi ninafikiri ni kwa sababu walikuwa wamelichukua Neno la Mungu na kulitangua Hilo, kwa mapokeo yao. Yesu alisema hivyo. Alisema, “Nyinyi, kwa mapokeo yenu, mmelitangua Neno la Mungu.” Hiyo ni kweli. Halikuwa na nguvu, kwa sababu iliongeza na kuingiza ndani ya Hilo mapokeo yao. Na wakati. . .

⁸⁵ Huwezi kuongeza chochote kwenye *Hilo*. Huwezi kuondoa chochote kutoka kwenye Hilo. Hilo ni, hivyo ndivyo tu Hilo lilivyo. Hivyo ndivyo Mungu alivyolihifadhi Hilo. Hatuwezi kuongeza kanuni za imani na mafundisho ya sharti na

kadhalika, kuingiza katika Hilo. Hilo halihitaji usaidizi wowote. Hilo ni—hilo ni Yeye, hilo ni Yeye katika njia ya maandishi.

⁸⁶ Nalo Neno ni Mbegu. Na mbegu katika aina nzuri ya udongo itakua, usipoichimbua kila asubuhi kuona kama imekua au sivyo. Wewe ipande tu, uikabidhi kwa Mungu, na uiache hapo. Hiyo ndiyo njia ya kuiacha ikue, kuiacha tu Hiyo jinsi ilivyo ardhini. Na hapo ndipo Hiyo inapopaswa kuwa, udongo wa moyo wako. Imani inaimwagilia Hiyo maji, kila saa, ikisema, “Kama Mungu alisema hivyo, ni yangu!” Hiyo ndiyo njia ya kuifanya.

⁸⁷ Kwa hiyo ulimwengu mzima wakati huo ulikuwa unaporomoka kama ulivyo leo hii, kila taifa lilikuwa likitazamia mtu fulani ku—kuwashikilia kutokana na msiba huu uliokuwa karibu kuipiga dunia, na kujaribu kuwashikilia pamoja. Mataifa yalikuwa yanatazamia kitu fulani, na—na kila taifa lilikuwa linakitazamia, lakini walionekana kana kwamba hawakutaka kukubali kile ambacho Mungu aliwatumia. Walikuwa wanaomba wapate mtu, masihi, ambaye angeweza kukanyagia mbali mataifa yote mengine, na Mungu akawapa Mtoto mchanga. Wakiomba Jenerali, na kupata Mtoto mchanga! Mungu alijua kile walichohitaji. Aliwashusha.

⁸⁸ Hivyo ndivyo Mungu hufanya, Yeye hutushusha wakati tunapodhania tunajua kitu fulani. Kama vile Yeye alivyomwambia Ayubu, “Una hekima nyingi sana, ulikuwa wapi wakati niliweka msingi wa ulimwengu, wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha? Ulikuwa wapi, Ayubu?” Mbona, hekima yake ilishindwa, unaona. Na Mungu hutushusha tunapoanza kufikiria kwamba sisi ni kitu fulani mashuhuri. Wakati tunapofikiria shirika letu ndilo la pekee, Mungu atarudi kutoka kwenye kitu kisichokuwepo, ainue kitu fulani na kutudhalilisha kwa hicho. Hiyo ni kweli. Yeye daima hulifanya hivyo. Naam.

⁸⁹ Unaona, waliomba wapate Jemadari, na wakampata Mtoto mchanga. Mungu alijua kile walichohitaji. Hiyo ni kweli. Waliomba wapate Jemadari, na kupata Mwokozi. Ingawa walidhania waliokoka, lakini kuzuriwa kwao na Mungu kulionyesha kwamba hawakuokoka.

⁹⁰ Labda hilo hasa ndilo shida ya leo hii. Ulimwengu unadhania wameokoka, kwa kujiunga na kanisa, bali wanahitaji Mwokozi vile vile tu leo. Kama hiyo siyo picha ya ulimwengu leo hii, siujui ulimwengu.

⁹¹ Hivyo karibu tu ndivyo ulivyo kwenye Krismasi hii, tena tunakuta kitu kile kile, ulimwengu unaporomoka. Ukienda kwenye *hiki*, hicho kimekwisha. Ukienda kwenye *hiki*, hicho kimekwisha. Imefikia hivyo ili kwamba tuweze kuja kwenye *Hili*. Unaona, i—inaondoa mihimili yote kutoka chini yetu, ili kwamba iweze—iweze kutubidi kuja kwenye tegemeo la pekee lililopo, na hilo ni Uzima wa Milele.

⁹² Unatazamia sasa leo hii, kama ulivyokuwa wakati ule, mfumo fulani wa kuushikilia pamoja. Kama ilivyokuwa wakati ule, sasa tena unaporomoka. Na ulimwengu wa kidini wakati ule ulikuwa unatazamia Masihi aliyeahidiwa kufanya hili.

⁹³ Na Mungu hutimiza ahadi Yake. Yeye kamwe hakosi kutimiza ahadi Yake katika nyakati zote. Wakati ulimwengu ulipokuwa unaporomoka, katika wakati wa Nuhu, Mungu aliwatumia nabii mwenye nguvu. Walifanya nini nalo? Walilikataa. Nabii ni kitu gani? Yule ambaye hujiliwa na Neno, ni Neno la Mungu tena. Katika wakati wa—wa Nuhu, walilituma. Katika wakati wa Musa, mfumo wote ulikuwa unaporomoka, walimtuma nabii. Katika wakati wa Eliya, mfumo wote ulikuwa unaporomoka, walimtuma nabii. Kila wakati, wakati ulimwengu ukiingia kwenye machafuko haya, wanamtuma nabii. Ndipo basi kwenye Krismasi hii ya kwanza, Yeye alilituma Neno katika utimilifu Wake, unaona, Neno! Sehemu ya Neno ndani ya nabii, nabii alikuwa na Ujumbe kwa ajili ya wakati huo, naye akatokea.

⁹⁴ Walipewa nabii, na wao walifanya nini na wao kila wakati? Waliwapiga mawe (hawakukubaliana na mifumo yao) na kuwaua. Yesu alisema, “Mnapaka chokaa kuta za manabii, makaburi, na baba zenu waliaweka humo ndani. Na nyinyi mnashuhudia kwamba, kwamba nyinyi ni watoto wao.” Unaona, wanafanya hivyo. Ni vibaya sana, lakini huo—huo ndio ulimwengu. Unaona, daima, Mungu hutuma Neno Lake, na hekima hujaribu kulipinga Neno.

⁹⁵ Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwenye mwanzo. Kitu kile hasa kilichoanzisha mfumo wote wa dhambi kilikuwa ni kwa sababu mtu fulani, Hawa... Shetani alileta mpango ulio bora kuliko wa Mungu; alileta hekima. Wanakula kutoka kwenye mti wa maarifa.

⁹⁶ Hekima daima hukupeleka mbali na Mungu. Imani hukurudisha kwa Mungu. Humjui Mungu kwa hekima yako kubwa. Wewe... Haifai kitu. Ni ya ulimwengu. Ni upumbavu kwa Mungu. “Lakini ilimpendeza Mungu, kupitia upumbavu wa kuhubiriwa Neno Lake, kuokoa waliopotea.” Unaona? Kwa hiyo Mungu daima alitumia kitu kipumbavu na duni.

⁹⁷ Wakati Yeye alipowaita wanafunzi Wake, ikiwa Yeye angemchagua Kayafa na makuhani mashuhuri ambao walikuwa wamefunza kwa ajili ya wakati huo, kulikuwa na kitu cha kujivunia. Walikuwa na digrii yao ya udaktari na kila kitu. Bali Yeye anashuka chini na kuchukua watu wasio na maarifa, wavua samaki ambao hawakuweza hata kusoma jina lao wenyewe au kuandika jina lao wenyewe, kusudi Yeye aweze kuchukua kitu duni na kufanya kitu kutokana nacho.

⁹⁸ Hata Mtakatifu Paulo mashuhuri alisema ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujua, kusudi aweze kumpata Kristo. Aliambia

kanisa la Korintho, “Sikuja kwenu na ufasaha wa maneno na hekima ya ulimwengu huu, kwa sababu mngejenga imani yenu katika hilo.”

⁹⁹ Pia tazama, leo, watu hawataki mchungaji isipokuwa anaweza kuzungumza tu vizuri na kufanya nomino zake zote na viwakilishi nomino. Na kama hilo liko hivyo, nisingeweza kuingia katika mimbara yoyote, maana hata sijui tofauti kati ya nomino na kiwakilishi nomino. Na jambo pekee nijualo, ni, ninamjua Yeye. Na hayo ndiyo yote ninayojali kujua, kwa kuwa Yeye ni ninii yangu—Yeye ni Nomino yangu na Kiwakilishi nomino, Yeye ni Uzima wangu. Sasa kitu tunachotaka kujua ni Yeye. Lakini unaona mfumo wetu wa dini umeingiza mfumo wa kielimu, na kuchukua mahali pa Roho Mtakatifu. Hilo ndilo limefanya.

¹⁰⁰ Sasa, katika siku za Nuhu, siku za Musa, waliwatumia manabii, na wao walifanya nini? Waliwapiga mawe, wakawaua, wakawakata kwa msumeni vipande vipande, wakawateketeza, njia yoyote kuwaondolea mbali, kuwaondoa kwenye mikono yao.

¹⁰¹ Yesu alifundisha kile kizuri sana, akaleta methali, wakati Yeye aliposema, “Kulikuwa na mtu, mtu mashuhuri aliandaa . . . alikuwa na shamba la mzabibu na kuweka wafanyakazi katika hilo. Naye akamtuma mtumishi, nao wakamwua. Akamtuma mtumishi mwingine, nao wakamwua, na kadhalika.” Kisha kasema, “Hatimaye kasema, ‘Mimi, nitamtuma mwana wangu, nao watamheshimu.’ Nao wa—wafanyakazi wa shamba la mzabibu wakasema, ‘Huyu ni mrithi, hebu tumwue.’” Huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu ambaye Yeye alimtuma.

¹⁰² Kuwatuma manabii! Kutuma Neno Lake; Neno, Mungu! Kumbukeni, kila kizazi kinachoanguka, lipo jambo moja tu liwezalo kuweka ulimwengu huu pamoja, hilo ni Neno la Mungu!

¹⁰³ Ulimwengu huu uliumbwa kwa Neno la Mungu. Limeunganishwa pamoja na Neno la Mungu. Hilo ndilo kitu pekee kitakachowahi kuweka Hilo pamoja, ni Neno la Mungu, kwa kuwa Waebrania ilisema, “Tunafahamu kwamba ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu.” Watu wanalishuku Neno la Mungu, na vumbi hasa unalokalia ni Neno la Mungu likidhihirishwa. Viti hasa mnavyokalia ni Neno la Mungu likidhihirishwa. Mungu hulinena, nalo halina budi kutukia, kwa sababu ni Ne—Neno la Mungu.

¹⁰⁴ Sasa kitu pekee kiwezacho kukiweka pamoja, hakitakuwa mfumo wa kisiasa, hakitakuwa ni U.N., hakitakuwa chochote cha mashirika haya. Kitakuwa ni Neno la Mungu linaloweka u—ulimwengu pamoja. Hicho ndicho kitu pekee ambacho ninaweza kupendekeza leo hii, kuuzuia ulimwengu usiporomoke sasa

hivi, ni, kurudi kwenye Neno la Mungu. Hilo ni mpango wa Mungu, daima.

¹⁰⁵ Katika bustani la Edeni, Shetani alikuja na kumwambia Hawa, alisema, “Unapaswa kula tunda la mti.”

Ndipo yeye akasema, “Lakini Bwana alisema tusile.”

¹⁰⁶ Akasema, “Sasa, loo, hakika hamtakufa.” Unaona, alijua mradi tu watu walibaki wamekingwa!

¹⁰⁷ Hili ndilo tunalopaswa kukingwa nalo, ni Neno. Unaona, tumezungukwa na Neno. Neno liko ndani yako; Mungu ndani yako, kukuzunguka wewe. Popote uendapo, ni Neno, Neno! Mweke Yeye daima mbele zako. Kumbukeni, mtambueni Yeye kila mahali. Sasa, wakati Hawa na Adamu walipotembea namna hiyo, hakukuweco na kifo. Mwanaume au mwanamke ambaye anatembea namna hiyo sasa, hakuna kifo kwao, wanao Uzima wa Milele wakati wewe—wakati unapozungukwa na kuhifadhiwa na Neno.

¹⁰⁸ Sasa tazama, hekima huja ili kulipinga Neno, na, inapofanya hivyo, Hawa alivunja kizuizi hicho. Basi wakati Shetani alipogundua kwamba hapo palikuwa ndipo mahali angaliweza kuipiga jamii ya wanadamu, hapo ndipo hasa ambapo ameipiga kila wakati. Hata katika roho ya upinga Kristo, karibu sana hata ingewadanganya Wateule wenyewe katika siku za mwisho, yeye huja katika umbo la dini. Sasa hakuna kitu kama chama cha kikomunisti kumpumbaza mtu yeyote; wao ni—wao ni wapinga Mungu, kwa kuanzia, lakini huo sio upinga Kristo. Upinga Kristo ni dini, karibu sana hata ingemdanganya Mteule mwenyewe.

¹⁰⁹ Mwangelie Yudasi Iskariote, alitembea moja kwa moja pamoja na Kanisa, na kumkiri Kristo. Alifanya kila kitu ambacho wale wengine walifanya, akaenda nje na hata kufukuza pepo, na kurudi akishangilia, pamoja nao. Kwa usahihi, Mathayo 10. Lakini ilipofikia mahali kwenye Pentekoste, kupokea Uzima wa Milele, alionyesha rangi zake.

¹¹⁰ Na hapo ndipo inapofikia leo hii. Ibilisi hukuacha uwe na kujiunga kwote na kanisa unakotaka. Lakini ikifikia wakati ambapo unampokea Roho Mtakatifu, yeye atapaza tu sauti, “Ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha,” ama kitu fulani. Ha—hataki chochote kuhusiana na Hilo. Basi Yudasi na mfumo wake anaweza kufuata moja kwa moja hadi wakati huo. Maana, hapo ndipo Yudasi alipoudanganyia ulimwengu ule, kufikia mahali hapo, bali asingeweza kufanya hilo huko. Huyu ni Mteule papo hapo. Sasa, anaweza kuja karibu hivyo, bali yeye—bali yeye hawezi kuja njia yote. Kwa sababu, kama angefanya hivyo, angetuwa ndugu yako basi, kwa hiyo hawezi kufanya hivyo.

Mtu fulani alisema, “Unajua, ibilisi alinipata.” La, kamwe hakukupata.

¹¹¹ Wewe ulienda nje kumfuata. Kamwe hakuvingia ndani na kukupata. Maana, “Wewe umekufa, na uhai wako umefichwa katika Mungu, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu.” Njia ya pekee angaliweza kuingia Mle, ni njia ile ile uliyoingilia. Kwa hiyo yeye alikualika tu, nawe ukatoka nje kwenda kwake. Ni hayo tu. Unaona? Si kwamba yeye aliingia ndani kukutafuta. Hawezi kuingia Humo ndani, kwa kuwa wewe uko ndani ya Kristo, umeifia nafsi yako. Amina. Sijisemei amina mwenyewe, lakini hilo linamaanisha “na iwe hivyo.” Na ni—ni—ninajua ni kweli, nimepitia hayo na ninajua kwamba ni kweli. Ni kupita kutoka mautini kuingia Uzimani, kumpokea Kristo ndani yako. Vema.

¹¹² Sasa tunaona, basi, kwamba u—ulimwengu wa kidini katika siku hiyo ulikuwa unaporomoka, na wao—wao daima walikuwa wamefanya hivyo hapo kabla. Na kwa nini? Ni kwa sababu kwamba manabii wajao, na Masihi ajaye, hawakutimiza maelezo yao, sharti lao la kitheolojia kwa ajili yake. Wao . . . Haikutimiza.

¹¹³ Na hivyo ndivyo ingekuwa leo hii. Hii ndiyo sababu, ninaamini, leo hii, kwamba sisi—sisi tumedumaa katika siku hii, kwa sababu, katika huduma ya Mungu, kwa sababu hiyo, hata katika makanisa, kamwe haifikii hasa masharti ya kile walichowazia kwamba inapaswa kuwa. Wanawazia kwamba, “kunapaswa kuwa na wakati ambapo mambo *fulani-fulani* yatatendeka,” ndipo—ndipo basi wakati kiini chake hasa kinaposhuka, vema, basi wao—wao wanakataa Hilo. Unaona?

¹¹⁴ Basi nini haja ya kuweka waya wa stima ukikataa dainamo? Unaona, hawawezi kupata nguvu zozote ndani yake, ni waya tu uliokufa. Hiyo ndiyo shida ya kanisa leo hii. Tumeweka nyaya zote juu; na kubonyeza kitufe, hakuna Uzima. Tunachohitaji kufanya ni kuunganishwa, hayo tu, sasa hivi. Unganishwa na Kristo, maisha yetu ya mhemko wetu, maisha ya nia yetu, kuunganishwa ndani Yake.

¹¹⁵ Unasema, “Vema, na—nakwambia, ni—ni—ninaamini mimi. . .” Huna ninii yoyote. . . Huna wazo lolote linalokuja. Na hiyo ni kweli. Unasema, “Nafikiri *hili*. Pia mimi. . .” Huna wazo lolote. Sina pia.

¹¹⁶ Biblia ilisema, “Acha nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yenu.” Na Yeye daima alikuwa kwenye shughuli ya Baba. Kwa hiyo hilo ndilo wazo pekee unalopaswa kuwa nalo, kile Mungu alichosema juu yake, si kile mtu mwingine alichosema. Bali kile Mungu alichosema, hicho tu ndicho kilichoko kuhusu hilo. Yeye alisema, “Acha neno la kila mtu liwe uwongo, na Langu liwe Kweli.” Unaona?

¹¹⁷ Hilo ndilo jambo la kukata ulimwengu kurudi pamoja, bali wao hawatapokea Hilo. Sasa tunajua hawatafanya hivyo, maana kamwe hawakufanya. Vema. Tunashangaa basi, kama jibu ni leo, kilio leo hii, ni kwa ajili ya usaidizi ili Masihi aje. Na

mimi ninaamini wakati mwingine kama tukiweza, kama Yeye angetuma Hilo, nashangaa kama hatungefanya jambo lile lile walilofanya wakati ule.

¹¹⁸ Siasa zetu zote, zote katika dini, na—na pia katika maisha ya shirikisho, na kadhalika, zimechafuliwa. Tulichafua ibada yetu na mitindo iliyobuniwa na wanadamu, iliyobuniwa na kutengenezwa na mwanadamu kutoshea kila dhehebu lililoko kwenye uso wa dunia. Kila mtu analo wazo lao wenyewe tena. Lazima ije tena kama ilivyokuwa katika siku ambapo Mungu alimwinua nabii mwenye nguvu, Isaya, kasema, “Sadaka zenu na kadhalika zimekuwa mnuko katika pua Yangu.”

¹¹⁹ Unaona, Israeli, kwanza, wakati Mungu alipowaambia kuchukua sadaka na kuenda kuitoa, mbona, lilikuwa ni jambo kuu. Unaweza kuwazia Myahudi akiteremka barabarani, akiwa na mwa—mwanakondoo, mwanakondoo mdogo mnene au fahali, au chochote alichokuwa. Ilikuwa ni Pasaka, na yeye anateremka, anaweka mikono yake juu ya sa—sadaka inayomwunganisha yeye mwenyewe, akijitambulisha mwenyewe na sadaka hiyo, wakati anapoweka mkono wake juu yake. Kuhani alimwua m—mnyama huyo, maskini mwanakondoo, chochote kilichokuwa. Na wakati maskini mnyama huyo alipokufa, akirusha miguu na kulia, damu ilirashia juu ya mikono yake. Naye mwabuduo katika unyofu alijua kwamba huyo anapaswa kuwa ni yeye, bali mwana-kondoo alikuwa anachukua mahali pake. Hiyo ndiyo Yehova alihitaji, kwa sababu ilikuwa ni mfano wa Kristo. Lakini wakati mmoja hiyo ilizidi, kuendelea mpaka ikawa desturi ya familia. Walimtoa sadaka mwana-kondoo vile vile tu, bali hakukuwa na unyofu kuhusu hilo. Mungu akasema, “Zinanuka katika matundu ya pua yangu.”

¹²⁰ Na leo hii! Miaka iliyopita tulizoea kupata watu katika kilindi cha unyofu na ibada. Na leo hii imekuwa madoido makubwa ya Hollywood, namna fulani tu ya muziki uliofunzwa; na wanawake juu kwenye jukwaa, huku nguo zao zimewabana vya kutosha, ngozi ikiwa nje, karibu hivyo, na kucheza huku kote jukwaani; hakuna unyofu, na karibu kuifanya tu aibu ya moja kwa moja inayochukiza, huku wakikiri Ukristo. Nashangaa ikiwa sadaka zetu hazijakuwa aina ya harufu mbaya katika pua Yake tena, tofauti zetu!

¹²¹ Ni aibu tu kwamba adui amewachukua wanawake wetu wa Marekani na kuwavua nguo, huko nje mitaani. Na, mbona, ni—ni fedheha. Si ajabu wavulana wadogo na wasichana wadogo, na kadhalika, wako katika hali kama hizo walizo ndani yake leo hii! Daima wanajaribu kujifananisha na mwanamke fulani hapa nje kwenye Hollywood, aliyeolewa mara nne au tano. Na yeye atajitokeza amevalia namna fulani ya ngu—nguo uchi, na maskini wasichana wote nchini wataiga hiyo. Ni chukizo jinsi gani! Hilo ni baya sana. Naam, bwana. Ni baya sana,

nalo limeingia kanisani. Sifa nzuri ambayo Mungu alimpa mwanamke, kuwa mama, imechafuliwa.

¹²² Na huo ndio uti wa mgongo wa taifa. Wewe vunja umama, na umevunja taifa papo hapo. Hilo ni jambo moja ambalo husaidia kulishikilia pamoja, uzazi halisi wa kweli.

¹²³ Nilikuwa nikizungumza na dereva wa teksu, tukija huku chini. Tulikuwa tunazungumza kuhusu watoto fulani watovu wa nidhamu huko juu. Na yeye akasema, “Nafikiri ni wazazi.”

¹²⁴ Nikasema, “Amina. Jamani, sijui wewe ni nani, lakini uko kwenye barabara ifaayo.” Tena nikasema, “Hiyo ni kweli.” Nikasema, “Ni vibaya sana kwamba wameondoa Biblia kutoka nyumbani, na kuwapa jozi ya karata.”

¹²⁵ Na hiyo ilianzia kanisani. Nilikuwa nimesimama kwenye lifti, dakika chache zilizopita; ndipo mwanamke fulani pale, akizungumza na mwingine, kasema, “Vema, unajua,” akasema, “hiki ni kitu cha kupendeza, kanisa letu linafanya karamu ya kadi,” na jinsi walivyokuwa wanaenda kuwa na namna fulani ya shughuli ya bata wa kutoa Shukrani, kwamba walikuwa wanaenda, kutoka kwenye kanisa la kiprotestanti. Loo, jamani! Kucheza kamari, bahati nasibu, karata, densi, loo, inapofikia wakati ambapo watu inawabidi kufanya mambo kama hayo, kutumbuiza kanisa!

¹²⁶ Kanisa, lililozaliwa upya, Roho Mtakatifu huburudisha Kanisa, na Uzima wa Milele. Unaona?

¹²⁷ Lakini watu, hawamtaki Huyo, kwa sababu ni wapenda anasa. Ni vibaya sana kwamba mambo yalitendeka jinsi ambavyo yametendeka. Muda mrefu uliopita, muda mrefu kabisa uliopita, sifa nzuri ya wanawake na vazi lao zuri limesujudu mbele ya madhabahu ya mungu-mke wa Hollywood. Ni kweli. Ni jambo la kusikitisha mno kwamba ulimwengu umefikia mahali kama hapo. Uti wa mgongo wa taifa umevunjika. Mvuto wa kijinsia unachukuliwa mara nyingi kuwa ni mtindo, wa kisasa; watu wanavalia, wakitoka nje mtaani. Unajua kile Biblia ilichosema?

¹²⁸ Nitakwambia, nilikuwa nikizungumza juu ya hilo, wakati mmoja, na kulikuwa na mhudumu mashuhuri aliyeniambia, alisema, “Mbona usiachane na wanawake kufanya hilo na kusema hayo?” Na mimi nikamwambia, nikasema. Kasema, “Unapaswa kuwafundisha jinsi ya kuwa manabii wa kike, na kadhalika, namna hiyo.”

¹²⁹ Nikasema, “Ninaendaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatasoma ABC zao?” Daima mwamini Kristo, unajua, A-B-C. Na kwa hiyo nikasema, “Unawezaje kufanya hilo?”

¹³⁰ Mambo haya yote yamekuwa tu ni lundo kubwa lililoingizwa kanisani. Ni vibaya sana inaingia miongoni mwetu sisi watu wa Kipentekoste. Loo, enyi watu, simameni! Wazieni. Huenda

ukaniita mlokole sasa, bali kwenye Siku ya Hukumu utanipa mkono. Na ni—ninakupenda kwa—kwa upendo wa kiungu. Nami ninawatakeni muwe sahihi, enyi rafiki. Nini haja ya kubahatisha kwa vyovyote juu ya mambo kama hayo?

¹³¹ Mama fulani aliniambia, kasema, “Vema, Bw. Branham, wao—wao hawaninii, wao...hiyo ndiyo aina pekee ya nguo wanazotengenezea wanawake.”

¹³² Nikasema, “Wangali wanatengeneza vitambaa, na kuuza cherehani.” Wewe—wewe, hakuna udhuru, unaona. Hiyo ni kweli.

¹³³ Tazama, na hebu niseme jambo moja tena, kama hili. Unajua, ukivalia namna hiyo, na mwenye dhambi fulani mtaani akutazame kwa njia mbaya, unaenda kujibu kwenye Siku ya Hukumu kwa kufanya uzinzi na huyo mwenye dhambi. Huenda ukawa safi kwa mumeo kadri uwezavyo kuwa, huenda ukawa safi kwa mvulana rafiki yako, mtiifu kadiri ujuavyo kuwa, bali machoni pa Mungu wewe ni kahaba wa mtaani.

¹³⁴ Unasema, “Je! hiyo ni kweli? Thibitisha hilo kwa Neno, Ndugu Branham. Ulisema tukuulize chochote, kama kilikuwa ni Neno.” Naam, bwana.

¹³⁵ Yesu alisema, “Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amezini na yeye tayari moyoni mwake.” Basi ukijianika mwenyewe namna hiyo, wewe ni msababishi wake. Hiyo ni hakika. Ijapokuwa usiwe na hatia katika nafsi yako, ulijianika mwenyewe kwa huyo mwenye dhambi namna hiyo. Anapojibu kwa ajili ya hilo, wewe utakuwa ndiye wa kuwa na hatia. Loo, jitafutieni nguo fulani mkajifunike, na mtende kama mama wa heshima. Hiyo ni kweli.

¹³⁶ Na nyinyi wanaume, nyinyi mtakaowaacha wake zenu kutenda jambo kama hilo, kuvaa nguo za namna hiyo, hivi huna heshima kwako ama yeye, yeyote wenu? Jamani, unamwacha mke wako aketi na kuvuta sigara nyumbani, na kuipuliza! Wewe ni kitu gani? Na halafu unajiita mwenyewe Mkristo? Loo, siwezi kuelewa hilo.

¹³⁷ Unasema, “Vema, sasa ngoja kidogo, ‘Kwa matunda yao mtawajua.’” Hilo ndilo ninalozungumzia, unaona. Hiyo ni kweli, kama unampenda Bwana kwa moyo wako wote!

¹³⁸ Unasema, “Vema, inanibidi tu kuvuta hizo sigara. Hiyo ndiyo raha yangu.” Ati raha yako?

¹³⁹ Raha yangu iko ndani ya Bwana. Raha yako iko ndani ya Bwana, kama ungeweza kufa kwa ulimwengu. Mungu ndiye furaha yangu. Yeye ni amani yangu. Yeye ni sadaka yangu. Yeye ni Mungu wangu. Yeye ni upendo wangu. Yeye ni yote, na yote ninayohitaji, na ninayapata ndani ya Kristo. Kuona kiu! Loo, jamani!

¹⁴⁰ [Dada fulani anaongea katika lugha nyingine. Ndugu Branham anatulia—Mh.] Iweni na kicho. Tunapaswa kungojea mambo hayo, mwajua. Wakati Roho anaponena, anapokatiza ujumbe na kunena namna hiyo, lazima kuna jambo muhimu linalokaribia kutendeka, unaona. [Kituo. Dada fulani anatoa tafsiri.] Amina. Amina. Nao watu wakasema, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”] Unaona? Unaona?

¹⁴¹ Sasa, kumbukeni, kama nimepata tafsiri vizuri, tunapaswa kuonya watu, unaona, Kuja kwa Bwana. Na hebu tuwaonye, pamoja na aina halisi ya maisha nyuma yake. Maana, huwezi kuzungumza na wanaume, ukiishi kwa njia yoyote, halafu uende umwambie. Anajua anaishi sawa na wewe, unaona. Hebu tuwe sawa na tuwe tayari, kwa sababu ninaamini Roho Mtakatifu anataka tujue mambo haya na kuwa tayari kwa ajili ya jambo hili kuu linalotayarisha kutukia. Naam. Naam, bwana.

¹⁴² Wakati, ulimwengu sasa unaporomoka. Mifumo yote inaporomoka. Ni kwa nini? I—inabidi ije kwa njia hiyo, unaona. Ni, “Sisi tunatazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni Wake ni Mungu,” na vitu hivi vyote vya duniani havina budi kuondoka njiani, kwa ajili Yake.

¹⁴³ Sasa tunapata kwamba Mungu aliahidi kukidhi mahitaji yetu yote tuliyohitaji, katika safari hii. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bali, kumbukeni, Yeye kukidhi tu hayo kwa masharti. Inatubidi kutimiza masharti Yake, kwanza. Tusipotimiza masharti Yake, Yeye hatatimiza—hatatimiza hali yetu. Inatubidi kufanya jambo lililo sahihi, kwanza, inatubidi kushuka chini na kujenga kuenda juu. Hiyo ni hakika. Hatuwezi kuanzia juu na kuteremka chini. Inatubidi kuenda chini na kujenga kuenda juu. Rudi chini. Sasa, Yeye atatimiza mahitaji yetu. Ahadi Zake zote zina masharti.

¹⁴⁴ Lakini tunajaribu kubadilisha Hii, kwa mapokeo yetu. Tunajaribu kumfanya Mungu kitu kingine. “Tunaenda kuingiza desturi yetu na kusema ni afadhali kidogo,” ama hivyo ndivyo watu wanavyojaribu kuliwazia.

¹⁴⁵ Sasa sizungumzii tu kanisa hili papa hapa, kundi hili la watu. Ninazungumzia ulimwengu. Inarekodiwa kwenye kanda hapa na itaenda kote ulimwenguni, kile tunachosema.

¹⁴⁶ Tunataka tupewe matakwa yetu, bali Yeye hutupatia haja zetu. Hiyo, hiyo ndiyo tofauti. Tunataka matakwa yetu, na Yeye hutupatia mahitaji yetu. Lakini Yeye anajua kile tunachohitaji. Na sisi tungeweza kwa hakika kabisa, ulimwengu ungeweza leo hii, kukubali Hilo kama Hilo lingekuja kulingana na desturi yetu. Loo, Wabaptisti wangependa kusema, “Ni kulingana na kile tulichoamini Hilo. Mnaona, nyinyi nyote mlikosea.” Wamethodisti wanasema, “Sasa nyinyi Wabaptisti mmekosea, Hilo ni kulingana na kile... Limekuja jinsi tulivyoliamini Hilo.” Bali ninawazia Hilo litakuja tofauti na kile yeyote wetu

anachowazia kuhusu Hilo. Hiyo ni kweli. Linaenda kuja vile Mungu amekusudia Hilo kuja, na haiko tu kabisa ndani ya mwanadamu kukatilia mbali kitu hiki na kusema iko hivyo. Sasa hivi ungeninii . . .

¹⁴⁷ Tunashangaa leo hii, kile, ni kwa nini karama na kadhalika haziko kanisani, zikifanya kazi jinsi zinavyopaswa kuwa. Mbona, karama zinawekwa kanisani, kutenga na kuondoa dhambi, kuliweka kanisa kuwa safi. Ni—ni dawa ya Mungu iliyotolewa kwa kanisa. Ni ninii ya Mungu . . . pia kiuu viini Chake ambacho Yeye huweka ndani ya kanisa, kuua na kuondolea mbali wa—wanyonyaji wote ambao—ambao hurarua kanisa. Tena—tena—tena Mungu hunyunyizia kanisa Lake kabisa, kwa Neno Lake. Na hiyo huweka m—mchwa wote nje, mnajua, kusudi kanisa liweze kukua, mche. Na Mungu anajua kinachohitajika kufanya hivyo. Vema, unasema . . .

¹⁴⁸ Ni kama tu m—mtoto mchanga anayelilia wembe wako, ulipokuwa unanyoa. Naye m—mtoto wako mchanga alikuwa akilia kwa sauti, “Nipe huo wembe, Baba! Nipe huo wembe!” Maskini mwanao, mwenye umri wa miaka miwili au mitatu, anapaza tu sauti, na kuruka juu—chini sakafuni, “Nipe wembe!” Vema, unajua bora kuliko kufanya hivyo. Vema, usingempatia huyo mtoto mchanga huo wembe. Hajui jinsi ya kuutumia.

¹⁴⁹ Na hiyo ndiyo sababu hatupati tena karama za Kiungu kuliko kile tufanyacho. Wanaisukumia mbali kwenye namna fulani ya desturi, huko kwenye dhehebu fulani. Hawajui jinsi ya kuishughulikia. Mungu anajua cha kufanya nayo. Vema, huenda ukasema . . .

¹⁵⁰ Maskini mvulana huyo huenda akakuambia, ulimnyima wembe, aseme, “Ninakuona ukiutumia, Baba.” Bali, unaona, wewe una umri mkubwa zaidi, unajua cha kufanya nao.

¹⁵¹ Na hivyo ndivyo wakati kanisa likikua kutoka kuwa m—mtoto mchanga anayeenda dede huku na huku, kufikia sifa halisi ya—ya wana na binti za Mungu, ndipo mambo yanaenda kuwa tofauti. Naam, bwana. Kanisa linapaswa kuwa likitenda kama wana na binti. Wakati tunapaswa kuwa walimu, inabidi tufundishwe.

¹⁵² Inanikumbusha. Ikiwa rafiki zangu weusi hapa usiku wa leo, ndugu zangu na dada, watasamehe tamko hili. Miaka iliyopita, huko chini Kusini, walikuwa wakiuza watu, wakati utumwa ulipokuwa ukiendelea huko chini Kusini. Na wao waliwachukua watu hao maskini, na wangewapeleka huko nje na kuwapiga mnada, kama vile lundo la motokaa za mtumba. Ungekuwa na bei ya kuuza.

¹⁵³ Maisha ya mwanadamu. Haikuwa ni mapenzi ya Mungu kuwa na mwanadamu yeyote akimtawala mwenzake. Mwanadamu alifanya . . . Mungu alimwumba mwanadamu, na mwanadamu akafanya watumwa. Sisi sote tumetokana na

mti ule ule. Mmoja anaweza kumpa mwenzake nyongeza ya damu, kama sisi ni manjano, weusi, hudhurungi, wekundu, ama chochote tulicho. Sisi sote ni jamii ya Adamu. Nchi tuliyoishi, ilibadilisha rangi zetu, haina uhusiano wowote nalo, si hata kidogo. Yesu alikufa ili kumwokoia mwenye dhambi, haijalishi alikuwa ni nani.

¹⁵⁴ Na kulikuwa na madalali waliokuja, walikuja hapo na wanguwanunua watu hao. Kama tu vile ungenunua mo—motokaa, kuja na kununua motokaa nyingi za mtumba; kuichukua, kuiuza mahali pengine. Wangukuja kwenye mashamba na kuwapata watu hawa maskini huko nje, na kuangalia kote, na kuona ni yupi aliyekuwa wafanyakazi wazuri, na wanaume na wanawake wakubwa wenye nguvu. Na wao wanguwauza, wachukue wanaume wakubwa wenye nguvu na kuwazalisha na wanawake wakubwa wenye nguvu, kama vile ungezalisha ng'ombe ama kitu kingine, kumpata mtumwa mkubwa zaidi, mnene. Sijui kile. . . Kuzimu kutajaa wa aina hiyo, ki—kitu kama hicho! Na hapa walikuwa, maskini mama mkongwe na watoto wake wachanga, wakilia, mume wake ameuzwa kwa mnada. Lilikuwa la kuchukiza.

¹⁵⁵ Ndipo muda si muda mwajua, dalali huyu mmoja alikuja kwenye shamba aliloambiwa, siku moja, naye alikuwa anawatazama watumwa. Ndipo akasema, “Una wangapi?”

Kasema, “Loo, tuna yapata mia mbili hapo nje.”

¹⁵⁶ Na kwa hiyo alimwangualia, na watu hao walikuwa na huzuni. Walikuwa mbali na makwao, wapendwa wao. Waliletwa kutoka Afrika hapa, na kuingizwa na Makaburu, na kuuzwa hapa chini Kusini, na wao—wao walijua wasingewahi kurudi nyumbani. Wao—wao walikwisha. Hawanguwahi kamwe kurudi. Na wao walikuwa na huzuni. Na wewe. . . Wasingeweza kuwafanya kufanya kazi, ilikuwa vigumu. Hawakuweza. Iliwabidi kuwacharaza, na kila kitu kingine, kuwafanya wafanye kazi, kwa sababu walijua wasingeweza kurudi nyumbani kamwe. Baba yao alikuwa huko, labda mama hapa na baba huko, na labda watoto hapa na baba yao mahali fulani. Loo, ni la kuchukiza.

¹⁵⁷ Ndipo siku moja dalali huyu alikuja na kutazama kundi hili la watumwa, na yeye akatambua kulikuwa na mmoja wa hao vijana watumwa hapo nje ambaye haikuwabidi kumcharaza yeye. Alikuwa na kifua chake mbele, na kidevu chake kimeinuliwa; alitembea kote, alikuwa mahali hasa alipotakikana. Ndipo dalali akasema, “Aisee, ninataka kumnunua huyo.”

Mwenyewe akasema, “Lakini yeye hauzwi.”

Kasema, “Kwa nini?”

Kasema, “Inanibidi kubaki na yeye.”

Akasema, “Yeye hapana shaka ndiye bosi juu ya wengine wote.”

Akasema, “La, la. Yeye si bosi.”

“Vema,” kasema, “labda unamlisha vizuri zaidi.”

Kasema, “Hapana, wote hula hapo nje manchani, pamoja.”

¹⁵⁸ Akasema, “Vema, ni kitu gani kinachomfanya kuwa tofauti sana na watumwa wengine?”

¹⁵⁹ Akasema, “Daima mimi nilishangaa hivyo mwenyewe, mpaka siku moja nikagundua.” Kasema, “Huko kwenye nchi ya wenyeji wake alikotoka, baba yake ni mfalme wa kabila. Na ingawa yeye ni mgeni, angali anajua yeye ni mwana wa mfalme. Yeye hujiweka kama mmoja.”

¹⁶⁰ Loo, kama sisi ni wana na binti za Mfalme, Mfalme wa wafalme, hebu tuweke tabia yetu kama Wakristo. Hiyo ni kweli. Naam, sisi ni wageni, sisi ni wasafiri na tu wageni hapa. Huu si ulimwengu wetu. Tunatafuta Ufalme ambao unakuja. Huku si kwetu. Ijapokuwa tuyumbishwe na kudhihakiwa, na ulimwengu, na kuitwa *hiki*, *kile*, na *kinginecho*, na “wa mtindo wa kale,” na yote namna hiyo, unajali nini? Hutaki kuwa ukijifaninisha mwenyewe na namna fulani ya bingwa wa sinema, ama bingwa fulani wa televisheni, au kitu fulani. Wewe ni binti wa Mungu. Wewe ni mwana wa Mungu. Hebu tutende kama Mungu. Sisi ni wana wa Mungu, tunajua, na sisi ni wana na binti za Mfalme. Hebu tabia yetu na iakisi Uwepo Wake, haijalishi jinsi inavyopata kuwa ngumu.

Hema au nyumba ndogo, kwa nini nijali?

Wananijengea ikulu Huko!

Pamoja na rubi na almasi, za fedha na dhahabu,

Hazina Zake zimejaa, Yeye ana utajiri usiosemeke.

Sisi ni wana wa Mfalme!

Pamoja na Yesu Mwokozi wetu,

Mimi ni mwana wa Mfalme!

¹⁶¹ Hebu tuenende kama Baba yetu. Tukijua kwamba, siku moja, tutaenda nyumbani kuwa pamoja na Yeye. Naam. Naam.

¹⁶² Wao, wao wanamtaka Masihi, bali wanamtaka chini ya masharti yao wenyewe. Naam, wanataka Mwokozi, walitaka, na wanamtaka sasa vile vile, kwa sababu ile ile, kwa kuwa madhehebu na siasa zimechukua mahali pa Roho Mtakatifu. Wahudumu, badala ya kuwa... Wengi sana wa hao wanaongozwa na si—siasa za kidini, badala ya kumwacha Roho Mtakatifu awaongoze. Unaona? Kanisa fulani litawapa matoleo mazuri zaidi kidogo, ama kitu fulani kingine, na hao wanaenda, kupata unyoya kwenye kofia yao, ama kitu fulani namna hiyo. Lakini, hiyo, hiyo ni mbaya sana. Tunapaswa kuongozwa na

Roho Mtakatifu. Mungu alimtuma Kiongozi halisi wa Kanisa, na huyo ni Roho Mtakatifu.

¹⁶³ Mfumo wetu wa elimu, makanisani mwetu, umetupeleka mbali na Uwepo wa Mungu. Ni vibaya sana kwamba tunaweka wavulana wetu (Ninazungumza kuhusu Wapentekoste sasa) huko nje kwenye seminari na kadhalika, kuwaangua kama kuku wa kiangulio. Hiyo ni kweli. Daima nilimhurumia kuku wa kiangulio, hakuinini—hakuanguliwa vizuri. Yeye hulia, na yeye hana mama wa kumwendea, ameanguliwa tu na mashine kubwa ya mfumo wa utawala. Hivyo ndivyo wanavyoonekana kuwa wanawatoa wahubiri leo hii, wakiwa na namna fulani ya digrii ya udaktari, na kumtuma katika kanisa. Na wakati mwingine huyo hajui zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti angeweza kujua kuhusu usiku wa Misri.

¹⁶⁴ Tunachohitaji leo hii ni dini nzuri ya mtindo wa kale, ya samawati ya anga, ya mwituni inayoua dhambi, na ubatizo wa Roho Mtakatifu kurudi ndani ya kanisa tena; dini ya samawati ya angani, iliyonyooka kabisa, itakasayo. Tunahitaji kutakaswa, na kuanza upya tena. Huo ndio Ukweli.

¹⁶⁵ Kanisa, sijarukwa akili. Huenda mimi ni mwendawazimu, kama nilivyosema jana usiku, bali na—najisikia vizuri hivi. Kamwe sikujisikia hivi vile vingine, kwa hiyo ni—ningependa tu kubakia hivi. Naam, bwana. Nilipoteza nia yangu; ilinibidi, ili kuipata nia ya Kristo. Kila mwaminio mwingine inambidi kupoteza, hiyo ni kweli, inambidi kupata nia ya Kristo, kwa kupoteza nia yetu wenyewe.

¹⁶⁶ Mfumo wa elimu umetupeleka mbali. Ninaishi katika mji wa chuo, ambapo Chuo Kikuu cha Arizona kiko huko. Na mimi nilikuwa ninasema, nikiwazia hili, sayansi inaweza kukufanyia nini? Wanaweza kuchukua kitu fulani, na kusema, “*hiki* kilikuwa miaka mingi sana iliyopita,” sasa waligundua haikuwa ni miaka mingi sana iliyopita. Hawajapata kitu kimoja bado, kisayansi, kinachothibitisha kwamba ulimwengu umewahi kuwa na uhai wowote juu yake, zaidi ya miaka elfu sita. Wanachukua mifupa, nao walikuwa wakichukua vipimo mbalimbali na kusema jinsi ilivyokuwa. Sasa, hawatakiri hilo. Profesa mkubwa hivi majuzi usiku, alisimama huko Arizona, na kusema, “Hawatakiri hilo, la, lakini waligundua kwamba umri wa mfupa umekuwa kwa sababu ya kloridi na kadhalika kwenye maji, na pia chumvi iliugeuza namna hiyo, na kuuchakaza. Kabisa si wakati uliofanya hivyo.” Amina.

¹⁶⁷ Neno la Mungu lingali linabaki lile lile, jana, leo, na hata milele. Hawawezi kamwe kuweza kuthibitisha Hilo kuwa sivyo. Hicho ndicho kitu ambacho kitashikilia ulimwengu pamoja; sio mfumo wa elimu. Chochote ambacho unachukua badala ya Hilo, ni huduma ya upinga Kristo; hilo ni kweli kabisa, ni kinyume na masharti ya Kristo. Kurudi kwenye Neno, na Kristo

ni Neno! Naam, bwana. Yeye ni Neno lililofanyika mwili na kukaa katikati yetu.

¹⁶⁸ Elimu kamwe haiwezi kutupatia Uzima. Elimu kamwe haiwezi. Sayansi haiwezi kutupatia Uzima. Ulimwengu hauwezi kutupatia Uzima. Kanisa haliwezi kutupatia Uzima. Theolojia haiwezi kutupatia Uzima. Kipo kitu kimoja tu kinachoweza kukupatia Uzima, hicho ni Kristo. Yeye ni Uzima, Uzima tele!

¹⁶⁹ Wakati fulani uliopita, katika jiji moja huko Kanada, nilikuwa nikipanda juu kwenye lifti. Na wao walikuwa na kundi la Wamarekani huko juu, na ilikuwa—ilikuwa ni namna fulani ya mkutano. Sitataja jina lake, kwa sababu huenda kukawa na mtu katika hicho chama fulani, hapa ndani, na mimi nisingetaka kuumiza hisia zenu. Lakini walikuwa wanapanda juu kwenye li—li—lifti, katika hoteli kubwa. Na nilikuwa na mkutano huko. Na ilikuwa vigumu, kuingia kwenye lifti, kwa sababu ya chupa za wiski na kadhalika. Ndipo nikamwambia m—mvulana wa lifti, nikasema, “Haya yote ni nini?”

¹⁷⁰ Akasema, “Wamarekani wametutembelea usiku wa leo.” Loo, jamani, wengi wa hao! Ndipo nikateremka chini.

¹⁷¹ Tulipoondoka kwenye—kwenye kituo ama ma—maskini eskaleta, ama lifti, hasa, na kuanza kutoka, kulikuwa na ukumbi, na kulikuwa na wasichana wawili waliokuwa wamesimama huko chini huku wamevalia vazi lao la ndani tu. Walikuwa na chupa ya wiski mkononi mwao, na walikuwa wanakunywa. Ndipo wakaanza kuteremka, na wanaume walevi wakitoka nje ya nyumba, wamelewa kabisa, ama vyumba vidogovidogo, wakijaribu kuwashika na kuvuta chini nguo zao. Na ilikuwa inaonekana ya kuchukiza. Ndipo wakashuka chini, na mimi nikarudi tu nyuma upesi katika ukumbi mdogo na kungojea mpaka wakapita, mlango mdogo, nao wakasimama mbele yangu. Na wanawake wenye sura nzuri, na walikuwa wamesimama hapo wakiwa tu wamevalia maskini sketi yao ya ndani, nguo zote walizokuwa nazo. Walichukua chupa hii, na kujaribu kumwagiliana. Mmoja alivuta vazi lake la ndani juu sana alivyoweza kulivuta, akatupa mguu wake hewani, na kupiga kelele, “Whoopee, haya ni maisha!”

¹⁷² Nisingevumilia zaidi ya hayo. Nilitoka nje, ndipo nikasema, “Dada, samahani. Haya ni mauti. Haya ni mauti.”

Akasema, “Njoo upate kinywaji.”

¹⁷³ Nami nikasema, “Ngoja kidogo tu.” Nikasema, “Ulisema hayo yalikuwa ni maisha.” Nikasema, “Haya ni maisha yaliyopotoshwa. Ni kwa nini unajaribu kufanya jambo kama hilo?” Nikaja kugundua... Nikasema, “Mimi ni mhudumu wa Injili. Mimi ni Mmarekani, pia. Na ninakuonea haya. Ninakuonea aibu wewe kujiita mwenyewe Mmarekani, na hapa juu namna hiyo.” Nikaja kugundua, mmoja wao alikuwa ni mwalimu wa shule ya Jumapili, na yeye akaanza kulia.

¹⁷⁴ Kwanza walianza kukimbia, na nikawashika wote wawili kwa mkono. Walikuwa wamelewa sana wasingeweza kuondoka. Nikasema, “Ngoja, tunaenda kuomba papa hapa.”

“Ipo njia inayoonekana kuwa sahihi.”

¹⁷⁵ Vema, unasema, “Wanakuwa tu na maskini raha safi.” Maskini raho safi? Bure! Kitu hicho hakininii... Sijali wewe ni mwalimu wa shule ya Jumapili kiasi gani. Ikiwa kitu hicho kiko moyoni mwako, Mungu hawezi kukaa ndani ya mahali hapo pachafu. Tunachohitaji ni uamsho wa utakatifu wa mtindo wa kale kuenea kanisani, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Naam, bwana. Hatufanyi hilo. Hilo halipaswi kuruhusiwa. Bali ni Wamerekani wakiwa na maskini “raha safi,” wakiweka mfano kama taifa la Kikristo. Loo, jamani! Mfumo wa elimu, huo si Uzima. Huo ni mauti.

¹⁷⁶ Ni kitu gani humfanya mtu kufanya hivyo? Ni kwa nini wanafanya hivyo? Ni kitu gani ambacho hufanya ulimwengu kufanya jinsi wafanyavyo? Kwa sababu wanakataa Hili. Pana mahali padogo katika moyo wa mwanadamu, ambapo humwonea Mungu kiu. Mahali padogo, mwanadamu aliumbwa kuwa na kiu. Umeumbwa namna hiyo. Hiyo ndiyo hukufanya kunywa pombe, hiyo ndiyo hukufanya kufanya mambo haya, ni kwa sababu kuna kitu fulani ndani yako ambacho hutamani sana kuridhishwa, kuona kiu. Na Mungu aepushe kwamba mtu atajaribu kuridhisha na kunyamazisha wito huo mtakatifu wa Mungu kwa kidadala ambacho ibilisi angempatia! Huna haki ya kufanya hivyo. Huyu ni Mungu akikuuta. Kitu hicho ni kiu ya mauti. Na ikiwa hutamchukua Kristo humo ndani kujaza mahali hapo, ibilisi atakupa kidadala cha mauti ndani yake. Hiyo ni kweli. Huna haki kufanya hivyo. Mwanaume yeyote au mwanamke anathubutuje kunyamazisha wito huo mtakatifu hapo ndani, wa Mungu akiita. Na kwa sababu hutapokea Huo, basi ibilisi atahakikisha umeridhishwa na kitu kingine.

¹⁷⁷ Hiki ndicho huiridhisha. “Neno la Mungu nimelificha moyoni mwangu, ili nisisende dhambi dhidi Yake.” Hiyo ni kweli. Mungu moyoni, ndicho kile kinatuliza swali. Naam, bwana.

¹⁷⁸ Sayansi haiwezi kukupatia Uzima. Elimu haiwezi kukupa Uzima. Dhehebu haliwezi kukupa Uzima. Shule haziwezi kukupatia Uzima. Taifa haliwezi kukupatia Uzima. Kanisa haliwezi kukupatia Uzima. Ni Mungu pekee anaweza kukupatia Uzima. Yeye ndiye wa pekee awezaye kufanya hilo.

¹⁷⁹ Sasa tunaona hasa kile ambacho nabii alisema kingetukia katika siku hii. Nabii, Paulo, katika Timotheo wa Pili 3, tunaona kwamba wakati ulikuwa unakuja ambapo kanisa lingekuwa, “Wakaidi, wenye kujivuna,” wajuaji, unaona, “wakaidi, wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiofanya suluhu, wasingiziaji, wasiotosheka, na wenye kudharau walio wema.”

Unasema, “Hao ni wakomunisti.” La. La.

¹⁸⁰ Hao ni wanaokiri kuwa Wakristo. Sikiliza, soma kifungu kinachofuata. “Wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana Nguvu zake; hao nao mjiepushe nao.” Tumeonywa kujiepusha na hao wanaokana Nguvu za ufufuo, wakikana kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kweli! Yeye ni yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸¹ Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, hata wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hiyo ndiyo kazi ya Roho Mtakatifu. Mradi tu Mungu angali anaita, Roho Mtakatifu angali hapa kujaza kila moyo wenye njaa ambao Mungu aliita.

¹⁸² Lakini sisi tunaweka kitu kingine badala yake. Tunajaribu kuridhisha hisia hiyo, kwa—kwa kujiunga na kanisa. Unaizima tu hisia hiyo, kwa kufanya hivyo. Huridhishwi na hiyo. Hiyo haitaridhisha.

¹⁸³ Kuna kitu kimoja tu kitaridhisha, hiyo ni wakati Kristo anapokuja katika maisha ya mtu, kwa kuwa Yeye amefanywa katika sura ya Mungu, na amefanywa katika kimo cha Mungu. Na Mungu hakukupatia safari hii hapa duniani, kuwa *hiki, kile*, au *kinginecho*, bali kuwa mwana na binti wa Mungu. Na hakuna kitu kingine kitakachoridhisha. Hicho ndicho kitu pekee kitakachoshikilia ninii wetu—ulimwengu wetu pamoja. Na usichukue uchumi wetu uliobuniwa na mwanadamu, bali chukua uchumi wa Mungu na njia Yake ya kufanya jambo hilo kupitia Neno Lake. Hilo litaushikilia pamoja.

Hicho ndicho Kifungo kifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Ni kama ule wa huko Juu.

¹⁸⁴ Hiyo ni kweli. Kile ulimwengu unachohitaji leo hii ni ufufuo mzuri wa wakati wa kale, wa Mtakatifu Paulo; na Biblia, Roho Mtakatifu kurudi tena; ambapo Roho wa Mungu anashuka miongoni mwa watu, na ishara na maajabu kuonekana, kama cheche kutoka kwenye fuawe. Naam, bwana, tunahitaji hicho. Hicho ndicho inatubidi kuwa nacho kuushikilia pamoja.

¹⁸⁵ Halafu tunamtarajia Mungu kukutana nasi katika mapokeo yetu. Loo! Kuuzuia ulimwengu usiporomoke, tunamtarajia Yeye kuja katika mfumo wetu.

¹⁸⁶ Sasa hilo hasa ndilo walilowazia kule nyuma, “Sasa kama Masihi akiya katika wakati huu, tunaye kuhani mkuu mwema, Kayafa. Tunaye Lavinski, makuhani hawa wote hapa, unaona, watu wema. Tuliwaelimisha, kuwaelimisha. Wanajua kile wanachozungumzia.”

¹⁸⁷ Lakini wakati Yeye alipokuja, Yeye alipita kila mmoja wao. Hata hakugusa mfumo wao. Mbali na hiyo, Yeye alisema, “Nyinyi ni wa baba yenu, ibilisi, na kazi zake mnazifanya. Enyi kizazi cha nyoka kwenye nyasi,” Yeye alisema, “Ni nani aliyewaonya kuitoroka ghadhabu inayokuja?” Angalia Neno la Mungu likijitokeza katika kemeo hilo. Loo, hakika halikuridhisha ladha yao ya kitheolojia. Na isingeridhisha leo hii, pia. Hairidhishi.

¹⁸⁸ Wakati walipomwona Yeye amesimama pale na kufanya ishara ya Nabii, kuonyesha kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, walisema nini? “Yeye ni Beelzebuli. Huyu ni roho mwovu juu Yake.”

¹⁸⁹ Yesu alisema, “Hayo ni makufuru. Na wakati Roho Mtakatifu ajapo, na unene dhidi ya Huyu, kamwe haitasamehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao.”

¹⁹⁰ Lakini mnaona mfumo leo hii? Ni kitu kile kile. Tuliunda mfumo wetu wenyewe, hiyo ndiyo sababu mfumo wetu kamwe hautaushikilia ulimwengu huu pamoja. Huenda wakamchagua Rais ama Abraham Lincoln fulani katika kila jimbo katika Marekani, na kamwe haitashikilia huo pamoja, mpaka turudi kwenye Neno la Mungu, kurudi kwenye Biblia ya mtindo wa kale yenye jalada nyeusi iliyo na Kweli. Hiyo ndiyo njia pekee tutawahi kumjua Mungu na kuuweka ulimwengu wetu pamoja, ni kurudi kwenye masharti ya Yesu Kristo, kurudi kwenye Fundisho Lake, kurudi kwenye Roho Mtakatifu tena akiongoza Kanisa.

¹⁹¹ Hiyo ndiyo sababu Kweli imeshughulikiwa vibaya sana katika siku hizi za mwisho, ni kwa sababu kwamba wakati Mungu anapojaribu kuingiza ndani mpango Wake, na watu tayari wamejiundia madhehebu na kuondoka katika huo. Wanajenga uzio ili kwamba Roho Mtakatifu hawezi kuingia mle ndani, kumweka Yeye nje. Tunamtaka Mungu atuokoe katika ha—hali hasa tuliomo. Hivyo ndivyo ninavyofikiri. . .

¹⁹² Enyi watu Wapentekoste, mlianza kwenye kitu gani? Hivi mliwahi kusoma Mtaa wa Azusa, misheni; je! mliwahi kusoma kabla ya Baraza la Jumla kuwahi kuanza? Watu wa Kipentekoste walijulikana kwa sababu walitoka kwenye madhehebu hayo, na kujitenga. Hicho ndicho walichokuwa. “Tokeni miongoni mwao,” walikuwa wakihubiri hilo nyakati zote, “mjitenge, asema Mungu. Ondoka kwenye mapokeo ya mwanadamu.” Basi alifanya nini? Aligeuka moja kwa moja na kurudi katika uchafu ule ule mliotoka. Sasa, mmetenganishwa; mmoja ni church of God; na mwingine, wewe ni *hili* au *lile*, *hili* au *lile*. Mmetangana, na kuzozana mmoja na mwenzake. Kuvunja kifungo hicho!

¹⁹³ Wakati nilipoingia hudumani kwa mara ya kwanza, niliwazia kila kitu kilichokuwa Pentekoste kilikuwa ni kundi moja. Nilikuja kugundua, walivunjika vibaya kama Wabaptisti.

Jambo nililofanya ni kusimama moja kwa moja katikati ya wote wawili, nikasema, “Sisi ni ndugu, hayo tu.” Kweli. Mradi tu mnatupiana risasi mmoja na mwenzake, Shetani hana haja kuwatupia risasi. Lakini acha kifungo hicho kivunjwe, na myatandaze mahema yenu huko nje, na kumwingiza ndani kila ndugu, ndipo, nawaambieni, jeshi kuu la Mungu litasimama katika Nguvu za Yesu Kristo, kurudi kwenye Biblia. Na mnazungumza kuhusu Kanisa kwa ajili ya neema ya unyakuo, itakuja kutimia wakati tunapoweza kurarulia mbali mapokeo yetu, kusahau mambo yetu yote ya kimadhehebu, na kurudi moja kwa moja kwenye msingi wa Neno la Mungu.

¹⁹⁴ Lakini tunataka Mungu atuokoe katika hali tuliyomo. Inatubidi kutimiza masharti Yake. Unaona, hatuninii, hatukutani nasi juu ya yetu; juu ya Yake! Tunataka Mungu atuokoe katika kitu kile kile ambacho—ambacho Yeye... Kimechafuliwa. Mruhusuni Mungu! Rudini kwenye Neno, na mpendane mmoja na mwenzake. Hicho ndicho kitu cha pekee ninachojua kufanya.

¹⁹⁵ Mungu hutupelekea manabii, na—na sisi huwaua, hasa kabisa kama Yesu alivyosema wangepanya. Ndipo tunakuta, baada ya karne moja ama mbili, ama miaka mia moja, au miaka hamsini, Mungu atatupelekea nabii, au mjumbe, na, muda si muda mwajua, tutamkosoa na kumwua. Halafu baada ya kitambo, baada ya yeye kufa, mwajua, kitambo, kanisa litaamka. Watafanya nini? Watasema, “Vema, tutajenga dhehebu juu ya hilo.” Hilo ndilo lililowafanyikia Methodisti, Baptisti, na wengine wenu wote, mlijenga dhehebu. Na jambo ni kwamba, baada ya yeye kufa, na ujumbe wake umekwisha, tunaishi basi katika mahali pengine. Ndipo unarudi pale nyuma, ujumbe wake kwa ajili ya siku hiyo, na unajaribu kurudi huko na kulipaka chokaa kaburi lake, wakati hapa Hilo linaendelea papa hapa kila wakati. Mnasahau majira!

¹⁹⁶ Kama tu vile wanadamu. Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa kile ambacho Yeye alifanya, na kumsifu Yeye kwa kile Yeye atakachofanya, na kupuuza kile ambacho Yeye anafanya. Hiyo—hiyo, hiyo ndiyo njia ya mwanadamu. Daima amefanya hivyo. Anafikiria kuhusu kile Yeye amefanya, anampa Yeye shukrani; anaamini Yeye anaenda kufanya jambo fulani *hapa* nje; bali anasahau Yeye anafanya hilo, kila wakati, papa hapa! Daima anapuuza hilo. Hiyo ni kazi ya ibilisi, kwake kulifanya hivyo. Naam, bwana.

¹⁹⁷ Mapokeo yetu! Naam, bwana. “Masihi,” wanasema, “ni kwa ajili ya kizazi kingine, kitu kama hicho. Alikuwa huko nyuma.” Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele!

¹⁹⁸ Katika kuja Kwake kwa kwanza, Yesu, ulimwengu wote ulichafuliwa na siasa na dini. Wote walikuwa wakililia Masihi.

Walitaka Yule aliyepakwa mafuta. Israeli walitaka kitu fulani, na Rumi ilitaka kitu fulani, na wengine wote.

¹⁹⁹ Ni jambo lile lile leo hii. Sisi sote, kila mmoja, tunataka mwanasiasa. Tunataka kitu fulani leo hii.

²⁰⁰ Sasa, leo hii, Urusi inataka masihi. Urusi inataka masihi ambaye atawapeleka mwezini upesi sana, afike huko kabla ya wengine wote kufika. Hicho ndicho Urusi inachotaka. Wanataka masihi wa aina hiyo, mwenye kipaji fulani, jamaa fulani ambaye ni—ambaye ni—ambaye ni mwenye kipaji katika sayansi, naye atajua jinsi ya kuvamia anga za nje na kuenda huko na kuipanda bendera ya Urusi kabla ya Wamarekani kufika huko. Loo, wao ni. . . Wanataka masihi wao. Wanajaribu wawezavyo kumkuza mmoja. Vema.

²⁰¹ Marekani ilifanya nini? Mnataka nini, Marekani? Mnalika kwa sauti kubwa kuliko wote. Mnataka nini? Mmekuwa mnataka mwe—mwenye kipaji aliyeelimika. Mmekuwa mkitaka mwenye kipaji katika siasa. Mlipata hicho. Ingawa iliwabidi kuvumbua ma—mashine ya kupiga kura isiyoaminika kupata hicho, bali mmekipata. Hiyo ni kweli. Ulimwengu unataka. . . Hicho ndicho unachotaka, sasa mnaenda kufanya nini na hicho? Mlitaka kuonyesha jinsi mlivyokuwa werevu. Hata mliwaweka kwenye televisheni, kuonyesha kwamba mmoja angeweza kumpiku mwingine, na mlivutiwa na hayo. Unaona? Mmekipata, sasa anaenda kuwaelekeza wa—wapi? Moja kwa moja kurudi Urumi, bila shaka. Mmekiona, sasa hivi.

²⁰² Enyi, kanisa, mnataka mwenye kipaji. Mnataka kitu gani? Mnataka kitu gani, kanisa linataka kitu gani? Mnataka nini? Mnataka mhudumu mwerevu, aliyeelimika kuinuka, anayeweza kushinda vizuri kuliko Billy Graham, kuwarudisha wote kwenye dhehebu lenu. Mnazo seminari na kadhalika, mkijaribu kuwaangua. Unaona, hiyo ni kweli. Huenda usifikirie kuwa hiyo ni kweli; bali, tazama, ma—matendo yako hunena kwa sauti kubwa kuliko maneno yako. Mnataka ninii—mnataka mwenye kipaji wa kidini, mtu awezaye kuwaongoza, dhehebu lenu, juu ya hao wote; kuwakanyagia mbali Wabaptisti, kuwakanyagia mbali Wamethodisti, kuwakanyagia mbali wa Umoja, kuwakanyagia mbali wa Utatu, kila kitu, kutembea juu ya yote hayo. Loo, mnaambaa tu ulimwengu wote, mkijaribu kumtafuta. Hiyo ndiyo aina mnayotaka.

²⁰³ Lakini je! mnajua kile mnachohitaji? Mnamhitaji Mwokozi, kile hasa mnachohitaji. Na hicho ndicho Mungu anajua mnahitaji, ni Mwokozi, na Yeye anawatumia Hicho. Lakini je! wanataka Hicho? La, bwana. Hicho hakiridhishi ninii yao—hakiridhishi ladha yao ya kikanisa. Kamwe hakifanyi kazi hivyo kwao.

²⁰⁴ Bali ulimwengu wote unataka mwenye kipaji wao. Sasa vipi ikiwa Urusi ilipata masihi wao, basi vipi kutuhusu sisi?

205 Unajua, Ujerumani ilipata wao, si muda mrefu uliopita, na wengi wenu enyi wavulana kutoka kwenye Vita vya Kwanza vya Dunia mnakumbuka hilo vizuri sana. Unaona, walimpata. Hamhitaji masihi wa namna hiyo. Kilikuwa katika njia isiyofaa. Kilikuwa ni kitu kisichofaa. Kilikuwa ni kinyume na Neno la Mungu.

206 Wazia tu, Napoleon, katika umri wa miaka thelathini na mitatu, alikuwa ameuteka ulimwengu, na kufa katika kushindwa. Alikufa katika kushindwa. Alikuwa ni mkataa vileo wakati alipoinuka kwa mara ya kwanza, na ufanisi wake mkubwa ulimletea; naye alikufa, mlevi wa pombe, makahaba elfu saba wakifuata jeshi lake. Naye alikufa kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu. Na yeye alijaribu kuuteka ulimwengu, lakini aliifanya kwa njia mbaya.

207 Lakini Yesu Kristo, kwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, alikuwa ameuteka ulimwengu, mauti, kuzimu, kaburi, na—na kupaa Juu. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Huyu ndiye Masihi wetu! Amina. Hakika. Wao daima, tunataka—tunataka Masihi, bali tunamtaka katika njia . . .

208 Itanibidi kuacha mambo fulani ambayo niliandika chini sasa, tunachelewa mno. Ina—inatubidi kuacha baadhi yake.

209 Lakini ulimwengu unataka—unataka masihi wao. Ulimwengu unataka mmoja. Kanisa linataka mmoja. Na vipi kama Mungu aliwatumia mmoja? Kama Mungu alimtuma Masihi, Yeye angekuwa kitu gani? Asingekuwa ni mwanasiasa wa kidini. Asingekuwa ni bingwa wa kiakili, kama ambavyo tungekiita. Loo, la.

210 Yeye angekuwa ni kitu gani? Angekuwa kama Waebrania 13:8, yule yule ambaye Yeye alikuwa. Daima amekuwa. Angekuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Hiyo ni hakika. Yeye alikuwa Neno la Mungu; Yeye ni Neno la Mungu; Yeye daima atakuwa ni Neno la Mungu. Hata ku—kutangazwa kwa Kuja Kwake, daima walikuwa manabii ambao Neno liliwajia. Hapa Neno lilikuja kwa ukamilifu.

211 Na sasa kama Yeye angekuja tena leo hii, Yeye angekuwa Ne—Neno la Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa, Neno la Mungu lililothibitishwa, Mungu akiishi miongoni mwetu. Huyu ndiye Masihi. Yeye aliahidi hilo. Amina. Yeye angekuwa ile Nguzo ya Moto tena. Yeye angekuwa Masihi yule yule aliyeongoza Israeli. Amina. Yeye angekuwa ni Masihi yule yule. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hakika, wangekataa Hilo kama walivyofanya daima. Hakika. Loo, maana wanataka kujenga taifa mashuhuri.

212 Tunataka kujenga mwili mashuhuri wa kanisa. Leo hii, tunawazia kuhusu, tunataka kanisa kubwa la jumla. Vema, mnaenda kulipata. Mlitaka kanisa lililoungana. Mnaenda

kulipata. Mnaenda kulipata. Kwa nini wanalitaka namna hiyo? Kama Masihi angekuja, Yeye asingeweza kuweka chochote namna hiyo katika utaratibu. Yeye angekipinga. Hakika, Yeye angekipinga. Lakini wao wanakitaka kwa sababu gani, ni kwa nini hakina budi kuja kwa njia hiyo? Wanataka mtu mmoja anayeweza kusimama na kuongoza kitu chote kwa imla. Mnaenda kukipata, hasa kabisa. Mtampokea, kwa sababu anakuja. “Mwingine atakuja, nanyi mtampokea,” Yesu alisema. Nao watafanya hivyo, watampokea. Ni kwa nini wanataka kufanya hivyo? Watu wanataka kufanya, mambo kwa njia yao wenyewe.

²¹³ Masihi angekuja, Yeye angevuta tu manyoya kutoka kwenu. Nena kuhusu mhubiri fulani kuwachuna ngozi wanawake na wanaume, Yeye angewachuna ngozi kwelikweli. Alifanya hivyo wakati Yeye alipokuja; Yeye alisema, “Enyi kizazi cha nyoka, nyinyi nyoka kwenye nyasi, nyinyi ni wa baba yenu, ibilisi.” Kama Masihi huyo angerudi katika wakati huu uliochafuka, Yeye angefanya jambo lile lile tena. Mungu angethibitisha kazi Yake kama tu Yeye alivyofanya mwanzo, pamoja na namna ile ile ya ishara na maajabu. Yeye hakika angefanya hivyo, kama Yeye angerudi tena. Kama tulikuwa na Masihi huyo, angekuwa tu kama Yeye alivyokuwa mara ya kwanza, kwa sababu isingeweza kuwa ni kitu kingine chochote. Biblia ilisema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Yeye daima ni Neno.

²¹⁴ Lakini sisi tunataka kitu gani? Tusingetaka Masihi wa namna hiyo. La, la. Tunataka kuwa kitu fulani kama ulimwengu. Na kile watu wanachojaribu kufanya, wanataka Masihi ambaye atawaacha kuishi na—na kufanya chochote wanachotaka kufanya, na kutenda kama ulimwengu na kuishi ulimwenguni, na bado washikilie maungamo yao ya Ukristo. Kweli. Huwezi kufanya hilo! “Ukipenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako,” Yesu alisema. Naam, bwana. Lakini huyo ndiye aina ya masihi ulimwengu unamtaka. Hiyo ndiyo sababu hawatampokea Masihi wa Mungu. Hautafanya hivyo.

²¹⁵ *Hili* ni Masihi Wake, hasa, Neno Lake ni Masihi Wake. Huyu Masihi ndani yako hufanya kazi ambazo Neno linasema linafanya. Huzalisha Kristo, maana Kristo yuko ndani yako. Uhai Wake uko ndani yako, na Huo hufanya hasa kile Yeye anachopaswa kufanya, kama Yeye alivyofanya daima; jinsi ile ile Yeye alivyofanya, mambo yale yale ambayo Yeye alifanya, kwa sababu Yeye ni yule yule. Huyu ndiye Masihi ambaye Mungu humtuma.

²¹⁶ Masihi ulimwengu unayemtaka, ni kuwaacha tu wafanye chochote watakacho, na kupita, “Loo, hilo ni sawa.” Loo, wanawake hawa kote nchini! Hawa, mnataka hiyo. Naam, wewe, wewe ulikuwa. Mnataka mavazi yenu ya Kifaransa na vitu vyote vikubwa. Mmepipata. Mnaye Ahabu mamboleo na Yezebeli, na

imewekea kanisa mtindo. Hiyo ni kweli. Mimi sizungumzi siasa. Ninasema Kweli. Je! mnajua taifa hili ni sawa tu na Israeli? Lilifanya jambo lile lile.

²¹⁷ Israeli waliingia na kuwafukuza wakazi kutoka kwenye taifa hilo, na kulichukua. Mungu aliwapa hilo. Basi wao walifanya nini? Waliwafukuza wakazi wa taifa hilo, na kulichukua. Kwanza, walikuwa na wafalme mashuhuri, kama Daudi na Sulemani. Ndipo baada ya kitambo, kukainuka mtu, jina lake Yezebeli... ama—ama Ahabu, naye akamwoa Yezebeli, na yeye alikuwa ni mmoja wa maskini hawa viruka njia waliojipaka rangi usoni. Na, wakati alipofanya hivyo, huyo mwanamke ndiye aliyemtawala. Alimwambia jambo la kufanya. Huenda alikuwa ndiye kichwa, lakini mwanamke alikuwa ndiye shingo na mwanamke alimwambia jambo la kufanya.

²¹⁸ Na ikiwa taifa hili halijafanya jambo lilo hilo, jambo lilo hilo! Tumeingia hapa ndani na kuwafukuza Wahindi. Tulikuwa na Washington na Lincoln. Lakini tuna nini leo hii, kwa kura zetu wenyewe, na siasa na kadhalika? Tuliweka mfumo, ambao tulitoroka na kufanya taifa kutokana nao hapa, tumeurudisha papa hapa ndani kwa sababu ni shauku ya watu. Kweli. Sasa, mimi si Mwanademokrasia wala Mrepublika. Mimi ni Mkristo. Kitu chote kimechafuliwa.

²¹⁹ Ninapiga kura yangu kwa Yesu Kristo. Amina. “Juu ya Mwamba huu nitasimama, nchi zingine zote ni mchanga unaodidimia.” Naam, bwana.

²²⁰ Marafiki, sisi hatujaahidiwa mfumo. Yesu asingekuwa na uhusiano wowote na mfumo. Hatukuahidiwa mfumo. Tuli ahidiwa (tuli ahidiwa kitu gani?) Ufalme! Unaingiaje katika Huo? “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Ufalme huu.” Ni Ufalme wa Mungu, Ufalme wa Uzima wa Milele, pamoja na Mfalme wa Milele akitoa Neno Lake la Milele, pamoja na watu wa Milele waliokusudiwa Uzima wa Milele. Yeye, Yeye ndiye Mfalme. Tumebatizwa katika Huo, tumeketi katika Utukufu wa Mbinguni.

²²¹ “Sisi tumekufa, uhai wetu umefichwa ndani ya Mungu kupitia Kristo.” Na si hayo tu, bali, “Tumefufuliwa pamoja na Yeye!” Tumefufuliwa kitu gani, katika mfumo, dhehebu, shirika? Tumefufuliwa ndani ya Ufalme wa Mungu! “Ufalme wa Mungu uko ndani yako.” Kwa nini? Mifumo hii yote iliyobuniwa na wanadamu haina budi kuanguka. “Si mara moja tena nitautikisa ulimwengu, bali nitatikisa mbingu. Na vitu vile ambavyo haviwezi kutikiswa, ndivyo vitakavyobaki. Na sisi tunapokea Ufalme, tunapokea Ufalme usioweza kutikisika au kusukumika.” Huo ndio Ufalme wa Mungu! Si mfumo, si gurutumu la kisiasa, si dhehebu, bali Ufalme! Amina! Na raia wake wamekufa kwa mifumo ya ulimwengu huu. Raia wake

wamekufa kwa madhehebu haya. Umekufa kwa mifumo hii ya kisiasa, na ni hai na umefufuka kwa Nguvu za Mfalme.

²²² Na sasa tuko katika Ufalme, tumeketi katika mahali pa Mbinguni pamoja na Mfalme wa Milele, tukifurahia Uzima wa Milele kwa Neno la Milele, tukienda katika Mbingu ya Milele, milele kuwa pamoja na Yeye. Haleluya! Tukiishi katika Uwepo wa Mfalme! Loo, ninampenda Yeye. Whiu! Nina furaha sana kuwa mmoja wao. Nina furaha sana kuwa nimekufa katika Kristo, ni hai katika Ufalme wa Mungu. Haya si Makao yangu; tunatafuta Ufalme. Tunatafuta Mfalme. Tayari tuko ndani ya Ufalme. Tunamtafuta Mfalme aje, na Mfalme upesi atakuja kwenye Ufalme Wake.

²²³ “Kwa kuwa tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Vitu hivi vingine vyote vinaporomoka. Marekani inaporomoka. Ulaya inaporomoka. Asia inaporomoka. Ulimwengu wote unaporomoka. “Bali sisi tuko katika Ufalme, Ufalme wa Milele, Huo hauwezi kutikisika,” amina, ambapo Krismasi ni kila siku, amina, kuishi katika Uwepo wa Mfalme. Utukufu! Haikubidi kubahatisha juu yake. Ni Kweli, Kweli ya Mungu, Kweli kamili ya Mungu. Jinsi ninavyompenda Yeye kwa ajili ya Hii! Jinsi Yeye alivyo mwema!

²²⁴ Wewe unayeketi hapo, ukiniangalia, maskini mwanamke huyo aliyevaa kofia nyeusi, anayeniangalia. Uko katika Ufalme, (unaamini hilo?) katika uwepo wa Mfalme. Ndio kwanza ufanyiwe upasuaji wa utumbo mpana. Hiyo ni kweli, sivyo? [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Na huo umekuwa ukikusumbua, umekuwa ukikusumbua; sahau huo. Unaenda kupona sasa. Kwa nini? Kuna uponyaji katika Uwepo wa Mfalme, katika Ufalme, “Kwa kuwa kwa mapigo yake sisi tuliponywa.” Amina. Amina.

²²⁵ Maskini ndugu mweusi anayeketi huko kwenye mwisho pale, aliyekuwa ameinua mikono yake, akiangalia huku na huku, akijaribu kunitafuta. Hukunipata; bali ulimpata Yeye. Kivimbe hicho kilichoko ubavuni mwako, kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atakiondolea mbali. Je unaamini hilo? Vema. Mungu akubariki. Amina.

Loo, Yeye si ni wa kupendeza, wa ajabu!

²²⁶ Kwa nini unatilia shaka? Usitie shaka. Una pumu, na unao ugonjwa wa moyo, unayo baridi yabisi, kila kitu. Unataka Mungu aite namba baada ya namba. Wakati Yeye anapokunenea, hilo ndilo. Kamwe usi—usitie shaka. Usisahau kwamba hiyo ni kweli. Mwamini Mungu, na wewe utapata kile ulichohitaji. Amina.

²²⁷ Mwanaume huyu anayeketi hapa, akiwa na pumu, maskini jamaa kutoka Norwe. Je! unaamini kwamba Mungu ataponya hiyo pumu na kukufanya mzima? Kama unaamini, Mungu atakufanya mzima. Amina. Kwa nini? Vema, unaweza kuupokea,

bwana. Hukujua ulikuwa na imani kiasi hicho, sivyo? Lakini Ufalme wa Mungu umekuja, na sisi tumeketi na Masihi, Masihi wa Mungu.

228 “Kwa nini unalisema hivyo, ‘Masihi’? Ni kitu gani Hicho, Ndugu Branham?”

229 Biblia ilisema, “Neno la Mungu lina nguvu kuliko ufalme wowote, kali kuliko upanga ukatao kuwili; ni Mtambuzi wa mawazo yaliyo niani, na makusudi ya moyo.” Ni Ufalme wa Mungu! Haleluya!

230 “Tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hivi mtamkubali Mfalme wakati Yeye akiwa hapa? [“Amina.”] Basi hebu tusimame kwa miguu yetu na kumsifu tu Yeye, kwa moyo wetu wote.

231 Bwana Yesu, tunakusifu Wewe, Ee Mfalme Mkuu wa Utukufu! “Sisi tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Naomba kwamba watu Wako, Bwana, waponywe, wakisimama, tukuza Jina Lako kuu, Baba. Tujalie hilo, Bwana. Warehemu watu. Tuna shukrani kwa ajili ya Ufalme huu, “Kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumebatizwa katika Ufalme huu usiotikisika.” Na sasa Mfalme wetu yuko miongoni mwetu, akithibitisha Neno Lake kwa ajili ya siku za mwisho; Nguzo ile ile ya Moto, Yesu Kristo yule yule, pamoja na ishara zile zile. Uhai ule ule uliokuwa ndani Yake uko ndani ya Kanisa. “Tunapokea Ufalme.”

232 Je! mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu tuimbe sifa Zake, “Nampenda, nampenda kwani Yeye alinipenda kwanza.” Hebu tuufanye usikike. Tupe sauti, ndugu. Kila mtu sasa pamoja, hebu tuimbe, *Nampenda*, tunapomsifu Yeye.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

233 Loo, jamani, hiyo si inasikika kama Mbingu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Nawaambia nini, hebu tuzoeane na wenyeji wetu wa Ufalme huu. Wakati tunapouimba tena, hebu tugeuke na kupeana mikono na mtu fulani karibu nasi, na tukisema, “Mungu akubariki, ndugu yangu, dada,” wakati tunapouimba, sote pamoja. Peaneni mikono, nyinyi nyote. Kwa sababu, “Kwa Roho mmoja sisi sote tuko katika Mwili mmoja,” tumeketi pamoja na Mfalme wetu.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²³⁴ Loo, si Yeye ni wa ajabu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Amina. Hebu tuuimbe tena sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²³⁵ Ni wangapi wanaojisikia kusuguliwa kabisa? Hebu tuone. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, jamani! Neno ni Chakula kwa nafsi yetu. Loo, jamani! Hebu tuuimbe tena.

Na . . . (Mungu awabariki!) Nampenda.



ULIMWENGU UNAPOROMOKA SWA63-1115

(The World Is Falling Apart)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 15 Novemba, 1963, katika Marc Ballroom kule New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org